Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 72 No. 166 | DHUL-QA'DAH 1432AH | OKTOBA 2011 | TABOOK 1390 HS | BEI TSH. 500

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na (kumbuka) Tulipomkalisha Ibrahimu mahali penye Nyumba ya kwamba usinishirikishe na cho chote, na uisafishe Nyumba Yangu kwa ajili ya wazungukao na wasimamao na wainamao, wasujuduo.

Na utangaze katika watu habari za Haji, watakufikia kwa miguu na juu ya kila mnyama mkondefu, wakija toka kila njia ya mbali; ***(Al-Hajj 22:27-28).***

Kiongozi wa Ahmadiyya duniani atoa mwito:

TUMIKIENI NCHI KWA SHAUKU

Na Jamil Mwanga Alton, London

Mkutano wa Mwaka wa 45 (Jalsa Salana) wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya uliofanyika, Alton, nje ya jiji la London maarufu kama 'Hadeeqatul Mahdi' yaani Bustani ya Mahdi. Mkutano huo wa kimataifa wa siku tatu ulivuta hisia za watu wengi kote duniani na kuhudhuriwa na wajumbe takriban 30,000 kutoka nchi mbalimbali.

Katika siku ya kwanza ya mkutano, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Duniani,Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a), alihutubia wajumbe mara mbili. Kwanza wakati wa Hotuba ya Ijumaa na kisha baadaye wakati wa sehemu yote ya kwanza ya Jalsa Salana. Aidha, kama sehemu ya ufunguzi rasmi wa tukio, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alipandisha bendera ya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya.



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) akiwahutubia waumini.

Awali kipindi hicho cha mchana kilitanguliwa na nasaha fupi kutoka kwa Jeremy Hunt ambaye ni Mbunge na Katibu anayeshughulikia Utamaduni, Olimpiki, Habari na Michezo wa Serikali ya Uingereza. Katika hotuba yake alisifu sana mwenendo unaooneshwa na Waislamu Waahmadiyya, hususan jinsi wanavyoshirikiana na jamii inayowazunguka. Bw. Hunt hususan aliisifu Jamaat kwa misaada inayoitoa kusaidia jamii na juhudi zake katika kutoa misaada ya kibinadamu katika maeneo mbalimbali duniani. Aidha, kwa niaba ya Waziri Mkuu, David Cameron na Serikali ya Uingereza aliitakia Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Jalsa Salana 2011 yenye mafanikio.

Katika hotuba yake ya mchana, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad alizungumzia kuhusu shabaha kubwa ya Jalsa Salana na alelezea pia kuhusu juhudi inayofanywa na Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya kufikisha mafundisho ya kweli ya Islamu duniani. Aliwataka wajumbe kuelewa madhumuni ya Jalsa Salana kuwa ni kuimarisha udugu, kujiongezea maarifa ya kiroho na kuondokana na matamanio ya kidunia. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa matamanio ya kidunia yasiwafanye muwe mbali na Allah na kwamba sifa ya muumini ni kuwa pamoja na kuendelea na shughuli za kidunia pia anamkumbuka Allah na hii ndiyo faida ya Jalsa kwamba mtu apate kuwa mchamungu na mwaminio wa kweli. Alisema muunganiko wa kidunia tofauti na ulivyo muunganiko wa kiroho, haumhakikishii mtu kupata mapenzi na ukaribu na Allah. Aliongeza kuwa kuna baadhi ya watu wanatumikia dunia tu bila kujitolea katika njia ya Allah lakini siku hizi katika Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya kuna mfano wa maelfu ya watu wanaojitolea wakiwemo pia watoto na akina mama. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa wapo watoto wanaomweleza kuwa tayari kujitolea fedha zao za kujikimu kwa ajili ya Allah. Aidha, baadhi ya watu baada ya kuhudhuria Jalsa wanaporejea makwao hujitolea zaidi kifedha. Alitoa mfano kuwa mara kadhaa amekuwa akipata barua watu wakimweleza kuwa wakati wa Jalsa walifurahia sana sala. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema zaka pia inatakiwa iende sambamba na sala.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a)

Endelea uk. 3

Kukosekana taqwa, chanzo cha ndoa nyingi kuvunjika:

Asema Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a.

Na Mwandishi wetu

Lajna (*Umoja wa akinamama wa Kiahmadiyya*) wametakiwa kuzingatia taqwa na kutanguliza dini mbele ya dunia kwa vile taqwa ndio mzizi wa wema.

Kauli hiyo imetolewa na Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alipokuwa akihutubia katika ukumbi wa akina mama wakati wa Mkutano wa Mwaka wa 45 wa Kimataifa kwenye viwanja vya Hadeeqatul Mahdi, Alton, Uingereza.

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a)

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema taqwa ambayo imetajwa katika aya za Nikah, inamsaidia muumini kujilinda na uovu na kwamba kama ikizingatiwa, dunia pia itafuata nyuma bila tatizo. "Libasi ama vazi la taqwa lenye kiwango linapofanikiwa huwezasha jamii kuepukana na madhara mengi", alisema Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) na kuongeza kuwa "Kama hakuna taqwa kwa wake na waume, basi hakuna uhakika wa kujenga vizazi vijavyo na jamii yenye amani".

Alisema kila mtu bila kujali dini yake, anapenda kuhakikishiwa amani kwanza pengine hata kabla ya wenzake.

Endelea uk. 3

Quran iliyopigwa marufuku yapanda bei Uganda!!!

Na Ali Khamis Mbambwa, safarini Uganda

Bila shaka wengi bado watakuwa wakimkumbuka aliyewahi kuwa Rais wa Uganda General Idi Amini Dada. Idi Amini aliitawala Uganda kati ya mwaka 1971 mpaka 1979, na kama ilivyo ada, kila mtu hukumbukwa kwa mazuri na mabaya yake. Wengi humkumbuka Amini kama mtu aliyekuwa mtemi, mbabe, dikteta aliyetawala kinyume cha sheria, alyekuwa akiendesha utawala wa ki-imla nk. Pia hukumbukwa sana kwa kisa maarufu duniani cha kuwafukuza watu waliokuwa na asili ya Asia nchini Uganda. Kwa asili Iddi Amini alikuwa muislam,nandiomaana alikuwa na marafiki wengi kutoka nchi za kiarabu au zile za kiisilam. Mfano mzuri ni ule wa vita vya Uganda na Tanzania ambapo Iddi Amini aliweza kupata msaada mkubwa tu kutoka nchi ya Libya chini ya utawala wa kanali Muammar Ghadafi, kana kwamba hiyo haitoshi, hata baada ya kutoroka nchini Uganda, Iddi Amini aliomba na kwenda kuishi uhamishoni nchini Saudi Arabia ambako aliishi huko mpaka kifo kilipomkuta.

Akiwa mtawalawa wa Uganda, Idi Amini alifanya mengi na kukataza mengi vile vile. Moja ya vitu vikubwa alivyokataza katika maswala ya dini, hususan dini ya Islam, ni kupiga marufuku Jumuiya ya waislam wa Waamadiyya. Inasemekana kuwa ilikuwa ni katika sherehe Fulani za maulidi, ndipo alipopiga marufuku dhehebu hili lililoanzishwa na Masih aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam wa Qadian (as) si hilo tu bali pia alipiga marufuku kuuzwa na kusambazwa kwa Quran Tukufu iliyotafsiriwa katika lugha ya Luganda. Tafsiri ambayo ilitolewa kwa

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KUNA SOMO KATIKA KUCHINJA

Dhul-hija ni mwezi mtukufu sana wa Kiislamu. Katika mwezi huu wenye bahati njema wanaenda Makka ili kutekeleza ibada ya Haji iliyofaridhiwa kwa kila Mwislamu mwenye mali na afya. Ibada mojawapo katika ibada za Haji ni kuchinja wanyama kama mbuzi, kondoo, ng'ombe na ngamia na hiyo inafanywa kwa kukumbuka sadaka iliyotolewa na Nabii Ibrahim; amani ya Mungu juu yake, miaka 4,000 iliyopita. Nabii Ibrahim (a.s.) alitaka kumchinja mwanaye Ismail (a.s.) kama alivyoona akifanya katika ndoto, lakini alipata amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu ya kuwa amwache Ismail (a.s.) na atoe sadaka mnyama. Tangu hapo Waarabu ambao ni wazao wa Ismail (a.s.) wakaendelea kutoa sadaka kama ukumbusho wa tendo la babu yao na baadaye jambo hili likawa sehemu maalumu katika ibada ya Hija ya Kiislamu. Hata wale Waislamu ambao hawafiki kuhiji wakiwa na uwezo wa kuchinja sadaka wanatakiwa kufanya vile ingawa hawakulazimika.

Je, Mwenyezi Mungu anafurahi kuona wanyama wakichinjwa? Au, damu ya dhabihu na nyama yake inamfikia kwa njia yoyote? Qurani Tukufu inaeleza ya kuwa sivyo.. Basi, kuna maana gani kutoa amri kama hii na hali Mwenyezi Mungu hali damu wala hatumii nyama? Majibu yake ni haya kuwa kwa ibada hii tumepewa somo kubwa lililo na maana sana. Sote twajua ya kwamba kila mwanadamu anazo tabia nyingine mbaya na nyingine nzuri. Tabia njema zinamwinua mtu juu na kumfanya awe sawa na malaika na tabia zilizo mbovu zinamvuta chini na kumfanya awe kama wanyama. Hasa tabia njema ndizo zinazompatia mtu utu-mwema na kumfanya astahili kupewa jina la- 'mwanadamu'. Tabia chafu zikizidi mtu anaonekana kama mwanadamu kwa sura tu lakini kwa undani huwa sawa na wanyama.

Basi sadaka hii inayotolewa na wenye kuhiji na wengineo ni kwa kumkumbusha; kila Mwislamu ya kuwa yeye anatakiwa kukuza tabia njema na kuhilikisha na kuangamiza tabia za unyama ndani yake. Kila mwaka Waislamu wanapewa somo hili ya kuwa wao watakuwa Waislamu hapo tu iwapo watajitahidi kuchinja unyama ulio ndani yao. Mambo mengi ya uasi, ukatili, ugomvi na mapigano hufanywa kwa sababu ya hiyo hiyo tabia ya kinyama. Kwa hiyo Mwislamu anafundishwa kila mara asiwe na sehemu ya unyama ndani yake. Katika mwezi wa Ramadhan unyama huo wadhoofishwa kwa kunyimwa vyakula saa za mchana na mnamo mwezi huu wa Dhul-hija Mwislamu anaonyeshwa mfano wa kuukomesha kabisa usiwepo tena.

Haiwezekani kusema ya kuwa leo watu wamestaarabika wala hawana haja ya kupewa amri kama hii ya kutoa sadaka; kwa sababu hatuna haja kwenda mbali kutafuta kama mambo ya ukatili yanafanywa au la. Hapa hapa petu wako baadhi ya watu ambao ni wanadamu kwa sura tu na undani wao umejaa mawazo na maazimio ya unyama. Sehemu nyingine za dunia pia zina watu wa namna hiyo. Duniani kote vitendo vya unyama zisivyosemekana vinaendelea kutendwa . Kwa mfano ni juzi tu tumesoma katika gazeti moja na kutangazwa kwenye vyombo vya habari juu ya kitendo cha kinguruwe ambapo mababa watano walikibaka kitoto cha miaka kumi na mmoja na wakakinajisi hadi kukiuwa. Hata wale ambao wanajiita watu wa dini pia hawachelei kuwadhulumu na kuwatesa wenzao. Kwa sababu za kidini pia maelfu ya watu wanauwa kila siku ulimwenguni bila kosa lolote. Basi hapana shaka dunia yetu ya leo inataka sana kupewa mafunzo haya ya Kiislamu ya kuwa watu hawatakuwa na amani kati yao mpaka wawe wameangamiza unyama na tabia zao za kinyama.

Furaha ya Idi ni kwa yule tu ambaye kwa hakika anaizunguka 'Nyumba ya Mwenyezi Mungu' (yaani anashika amri Zake tu) na anajizuia tamaa zake mbaya na nia zake za kuleta maudhi kwa wengine kana kwamba amezichinja na kuzing'olea mbali. Waislamu wasipofanya hivyo kuchinja kwao sadaka kutakuwa bure na furaha zao zote zitakuwa hazina maana hata kidogo. Tunatakiwa kuchunga watoto wetu pia wawe na utii mbele ya Mwenyezi Mungu kama alivyokuwa nao mtoto Ismail a.s. Hakuonesha ukaidi au kiburi alipojua ya kuwa Mwenyezi Mungu anataka atolewe sadaka. Ndiyo sababu aliokolewa na akapata uzima wa milele. Ama wale wanaofikiri dhambi zao zitabebwa na hao wanyama wanaochinjwa siku ya Idi watakosa wokofu kama wale wanaotegemea kifo cha mwanadamu na wanadhani wataokolewa na damu yake. Damu ya wanyama au ya wanadamu haitufikishi mahali popote ila kujitiisha nafsi zetu mbele ya amri ya Mwenyezi Mungu.

Quran iliyopigwa marufuku yapanda bei

Kutoka uk. 1

mara ya kwanza mwaka 1968 na kumalizika 1974. Mwaka huo huo 1974 ndio lilitolewa tangazo la kupigwa marufuku Jumuiya na uuzwaji wa Quran Tukufu katika lugha ya Luganda.

Akiongea na ujumbe wa Khudamul ahmadiyya kutoka Tanzania ulioongozwa na Sadri khuddamul ahmadiya wa Tanzania "Alli Khamis Mbambwa" uliokwenda kumtembea nyumbani kwake, mmoja wa waasisi na waliofanya kazi hiyo kubwa ya kutafsiri kitabu hicho kitakatifu nchini Uganda mzee Suleiman Mwanje, alisema kuwa Idi Amini alipiga mafuruku uuzwaji na usambazaji wa Quran tukufu iliyotafsiriwa katika lugha ya Luganda. Alisema kwa anavyoona yeye, Idi Amini kama yeye hakuwa na nia mbaya na Jumuiya wala kupiga marufuku uuzwaji wa Quran hiyo, bali ni shindikizo kutoka kwa mashekh wakubwa wa wakati huo nchini humo.

Hapa naomba nieleze japo kwa uchache tu utekelezwaji wa hii amri na shani ya M/Mungu iliyokuja baada ya amri hii. Inasemekana kuwa, utekelezwaji wa amri hiyo ulipangwa kuanza kwa kwenda kuchukua Quran Tukufu zote zilizokuwa makao makuu ya Jumuiya huko msikitini kwetu Wandegeya, Kampala – Uganda, tayari kwa kuzichoma moto. Siku hiyo askari wakiwa na sare maalum za kikazi, walifika msikitini huko Wandegeya na magari na kuanza kusombelea nakala za hivyo vitabu vitakatifu. Mzee Mwanje nae hakubakia nyuma, akiwa na gari lake, nae aliendelea kukusanya vitabu na kuweka kwenye gari yake mbele ya askari bila wao kumuuliza kitu.

Mzee Mwanje anasema kuwa kitu pekee alichoomba kuchukua kutoka kwa askari hao ni picha moja iliyokuwa na maandishi ya "*alaisa llah bikafin abdahu*" ambayo aliruhusiwa kuichukua. Yeye alichukua nakala hizo na kuzipeleka nyumbani kwake. Tafsiri hizo za Quran tukufu zilikuwa zimepigwa muhuri wa bei kuwa ni Ush. 80 kwa wakati huo. Baada ya zoezi la ukusanyaji vitatu hivyo kufanyika, basi vikahifadhiwa sehemu maalum chini ya ulinzi wa serikali.

Kukatokea mahitaji makubwa ya hizo nakala sambamba na mkutano wa kiserikali uliofanyika nchini, kutokana na kukosekana kwa fedha za kulipia posho kwa wajumbe wa mkutano huo wa serikali, ikaamuliwa basi zichukuliwe baadhi ya nakala ziuzwe na wajumbe wapate posho zao, ingawa jambo hili halikufanyika kiofisi lakini ndio ilivyokuwa baadae. Jambo la kushangaza zaidi ni kubwa bei ya halali ya Ush. 80 ikazidi hadi kufika Ush. 300 na hakuna hata nakala moja iliyowahi kuharibiriwa, zote ziliuzwa na mahitaji yakazidi kuwa makubwa maradufu.

Hii ni shani kubwa kabisa ya kimbingu, kwani hali ilikuwa tofauti kabisa na ilikuwa ikidhaniwa kutokea. Mzee Suleiman anasema kuwa kwa hakika ilikuwa ni ajabu sana. Nakala zote ambazo serikali ilizichukua ziliuzwa, na zile alizochukuwa yeye mbele ya askari nazo ziliuzwa kwa mpaka Ush 300, zaidi ya mara tatu ya bei ya asili. Alipofikia hapo, Sadri wa Tanzania, akamwabia kuwa M/Mungu alirudisha kwa Jumuiya mpaka zile nakala ambazo zilichukuliwa na serikali.

Anasimulia mzee Mwanje kuwa, kuna siku ilitokea msiba wa sheikh mmoja wa Jumuiya jijini Kampala. Masheikh wengi wakapinga kuzikwa kwa sheikh huyo kwa madai kwamba ni kafiri. Huyu sheikh pamoja na Uahmadiyya wake, alikuwa maarufu na alikubalika na wengi. Habari zikamfikia Rais wa nchi Iddi Amini, nae bila ajizi, akatoa amri mara moja kuwa huyo sheikh azikwe, tena akaagiza vikosi vya kijeshi kwenda kusaidia maandalizi na mazishi ya sheikh huyo.

Ni katika shughuli hiyo, ndio Iddi Amini alipotangaza kuwa Wahmadiyya ni Waislam kama walivyo Waislam wengine, na kuanzia hapo akatangaza kuwa Wahmadiyya wasisumbuliwe kwa lolote. Na kuwa mtu yeyote atakae wasumbua atachukuliwa hatua za kisheria. Si hilo tu bali alifikia hata kutoa namba yake ya simu kwa Waahmadiyya, kumpigia muda wowote kama watakuwa na shida yeyote. Hiyo ndio hali ilivyokuwa huko Uganda wakati huo. Hii inaonyesha mambo mengi. Lakini lililo kubwa zaidi ni kuwa pamoja na yote, bado Iddi Amini yeye kama yeye alikuwa na uzuri wake. Inawezekana baadhi ya wakati alifanya maamuzi magumu kidogo, lakini ukweli unabakia kuwa hivi sawa na hiyo mifano michache niliyoitoa hapo juu. Ama kwa hakika kila mtu atahukumiwa kwa yale aliyoyafanya.



Mzee Suleiman Mwanje (wa pili kutoka kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Majlis Khudamul Ahmadiyya Tanzania wakiongozwa na Sadr Khuddam walioshiriki katika Ijitimai ya Khuddamul Ahmadiya Uganda.

Tumikieni nchi kwa shauku

Kutoka uk. 1

alielezea jinsi matendo mema na maendeleo ya kiroho yalivyo silaha muhimu katika kuleta amani duniani. Sifa hizi kwa hakika zimekosekana kwa baadhi ya wale wanaojiita waislamu ambao wanawatesa Waislamu Waahmadiyya na makundi mengine. Alisema ingawa watu hawa wanasujudu na kurukuu lakini ibada yao haipo mbele ya Allah. Alisisitiza kuwa kuamini nguzo za imani hakumfanyi mtu kuwa mwaminio wa kweli bali ni lazima ajitahidi kutembea kwenye njia za uchamungu. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema si Qurani Tukufu wala Mtume Mtukufu Muhammad (Saw), aliyeruhusu aina yoyote ya mateso, msimamo mkali au ugaidi. Alisema, inasikitisha sana kwamba ingawaje Islamu inafundisha uaminifu katika kila nyanja, leo hii sehemu kubwa ya ulimwengu wa waislamu wamekuwa wakifanya vitendo vibaya zaidi kuliko watu wengine.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema muumini wa kweli lazima ajitahidi kupata taqwa na kumwogopa Allah. Sawa na alivyosema Masihi Aliyeahidiwa (as) kuwa kama lengo hili halipo basi hamna maana ya kuhudhuria katika Jalsa. Alisema muumini hatakiwi kunuia kulipiza kisasi bali kudhibiti hasira, kusamehe na kuwa na subira kwani hao ndio wanaopendwa na Allah. Kudhibiti hasira kuna malipo yasiyo na kifani. Matokeo yake ni kuwa mlango wa Allah hufunguka nao wanapata kuingia ndani. Alisema hasira na hekima kamwe haviwezi kukaa pamoja na kwamba kwa watu wa aina hii si rahisi kupata ushindi.

Akizungumzia kuhusu umuhimu wa uaminifu na mapenzi kwa nchi, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema:

"Waislamu Waahmadiyya lazima wawe na shauku ya kutumikia kwa ajili ya mafanikio ya nchi wanazoishi. Aidha, ni lazima daima wazitii na kuziheshimu sheria za nchi hizo."

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a.) alisema kwamba katika kipindi cha miaka michache iliyopita, kampeni ya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani kote kuhusu uaminifu, mapenzi na amani imesaidia kwa kiasi kikubwa kutangaza



Baadhi ya waumini wakifuatilia na kusikiliza hotuba ya Khalifa Mtukufu V (a.t.b.a) wakati wa Mkutano wa Mwaka wa Kimataifa wa 45, Uingereza kwenye viwanja vya Hadeeqatul Mahdi, Alton.

na kujenga uelewa kwa jamii.

Hata hivyo, kampeni hii sasa inaingia katika awamu ya pili ambapo ni jukumu la Jamaat Ahmadiyya kuufahamisha ulimwengu kuhusu madai ya mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) alidai kuwa ndiye Masihi Aliyeahidiwa aliyesubiriwa na dini zote, na madai yake yalithibitishwa kwa mafanikio na msaada mkubwa alioupata.

Akirejea tena maelezo ya Masihi Aliyeahidiwa (as) kuhusu shabaha ya Jalsa Salana, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alifafanua kuwa mkutano huu si mkutano wa kawaida kama ilivyo mikutano mingine. "Msichukulie mkusanyiko huu kama mikusanyiko mingine ya kawaida bali ni njia ya kupata mabadiliko (kiroho), hivyo kila mmoja ajichunguze kama anatimiza lengo la Jalsa.", alisisitiza. Aliwataka wajumbe kunufaika na Jalsa ikiwa ni pamoja na kusikiliza kwa makini hotuba zitakazotolewa na wataalam ili mkusanyiko huu usijekuwa sawa na bidaa.

Kipindi hicho cha mchana kilimalizika kwa maombi ya kimya. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alimwomba Allah ajaalie kupata baraka na fadhila za Jalsa sawa na matakwa ya Masihi Aliyeahidiwa (as), alisema pia tumwombee Mtume Mtukufu (Saw) na pia tuombee ushindi dhidi ya maadui na kwamba Allah amlinde kila Ahmadiyya. Baada ya maombi hayo maelfu ya waumini walitawanyika kuelekea maeneo mbalimbali. Baadhi walipiga kambi katika viwanja vya Hadeeqatul Mahdi, huku wengine wakielekea kwenye hoteli jirani walizokodi na wengine kuondoka. Hata hivyo, wote waliungana katika hisia na shauku ya kiroho inatokanayo na Jalsa Salana na hususan hotuba za Khalifa Mtukufu (a.t.b.a), Hadhrat Mirza Masroor Ahmad.

Matukio yote ya Jalsa Salana yamerushwa duniani kote kupitia televisheni ya Kimataifa ya MTA ambayo inaweza kutazamwa katika Sky 787 Uingereza. Pia matangazo hayo yanaweza kupatikana kwa njia ya intaneti katika MTA.

Kukosekana taqwa, chanzo cha ndoa nyingi kuvunjika

Kutoka uk. 1

Alisema kuwa Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kama mnataka kuwa na amani basi kuweni na sifa ya taqwa ili muwe katika ulinzi wa Allah. Kama mioyo yenu kweli ina hofu ya Allah basi mtakuwa mmepata taqwa na hamtafanya matendo yanayomwuudhi Allah wala kuwadhuru watu wengine na hivyo jamii itakuwa yenye amani. Ni muhimu kwamba tujenge amani katika jamii.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kutokana na athari ya utamaduni wa kimagharibi, baadhi ya wanawake wanafikiri kuwa uzuri ni kujipodoa. Hata hivyo, uzuri hasa tuliofundishwa na Allah kwa wake au waume ni kuvaa vazi la taqwa. Wake kwa waume wanatakiwa kulinda masikio, macho na ndimi zao. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa mara kadhaa amekuwa akiwakumbusha wake kwa waume kuhusu madhara yanayoweza kusababishwa na ulimi endapo hautatumika kwa uangalifu na makini. Mnatakiwa kuziba masikio ili amani ipatikane ambapo kama baba anakuwa ni mwenye hasira mama anatakiwa kukaa kimya. Hivyo hivyo, mama anapokuwa na hasira baba akae kimya, hali ambayo inaleta pia picha nzuri kwa watoto. Mtakapomwogopa Allah basi shetani atakuja mlangoni kama mwizi na hatoweza kuingia ndani. Timizeni wajibu wenu kwa viumbe kwani bila kufanya hivyo hamtoweza kutimiza wajibu kwa Allah. Kama mkitekeleza wajibu wenu kwa mujibu wa aya zinazosomwa wakati wa Nikah, mtaweza kutimiza matakwa ya taqwa na itakuwa pia ni njia ya kujenga vizazi vijavyo. Kila kitendo unachofanya kinatakiwa kisiwe tu kwa ajili yako bali kiwe kwa ajili ya kutimiza haki za Allah na za watu wengine.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa baadhi ya watoto huondoka nyumbani na kuamua kujichunga wenyewe kwa kuchoshwa na migogoro ya baba na mama. Hivyo, mkiweza kushikamana na taqwa itakuwa ni njia ya kulinda vizazi vijavyo.

Akizungumzia kuhusu kudumisha udugu kwa jamaa wa ukoo, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliwaasa mke na mume kuwa kama hawaangalii ndugu na jamaa wengine katika familia basi wajue kuwa Allah anawaona na ana habari ya yale wanayoyatenda. Alisema wakati mwingine kwa kukosa taqwa, lugha mbaya inatumika kwa ndugu, mathalani bibi, babu na jamaa wengine wa karibu. Alisema wazazi wanatakiwa kuwafundisha watoto kuheshimu ndugu wa ukoo kwa vile tabia ya wazazi pia huwaathiri watoto. Uhusiano na ndugu wa karibu unatakiwa uwepo kwa pande zote za ndugu wa mke na wa mume na si upande mmoja pekee.

Akielezea sehemu ya pili ya taqwa kulingana na aya zinazosomwa katika tangazo la Nikah, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alitaja kuhusu kusema kauli iliyo sawa/ukweli. Alisema kabla ya ndoa kila kitu kinatakiwa kuwekwa bayana ikiwa ni pamoja na masuala ya elimu na afya . Wakati mwingine vijana wa kiume huwafadhili mabinti au wake zao kutoka Pakistani, India na kwingineko. Hata hivyo, baada ya muda mfupi mmoja wao hubaini kuwa amedanganywa na matokeo yake ni kutengana, talaka au khula. Ingawa talaka imeruhusiwa lakini haifai. Vile vile, ndoa nyingine huvunjika kutokana na shinikizo la wazazi kulazimisha ndoa za watoto wao. Wazazi wanatakiwa kuweka wazi kwa wazazi wa upande mwingine endapo wamemlazimisha kijana au binti yao kuoa au kuolewa. Hivyo, kwa ajili ya kujenga amani katika jamii, inapaswa kudumisha ukweli na uaminifu.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alirejea hadithi inayosema: "Mkiacha kusema uongo, maovu mengi yataepukwa." Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliendelea kusema kumbukeni kushikamana na taqwa na kujichunguza kama mnazingatia katika kutekeleza Sala, haki kwa mume, jamaa wa ukoo, watoto na kwa viumbe wengine. Hivyo, kumbukeni kuwa kitendo chochote mnachofanya Allah ana habari nacho. Ikiwa kweli mnataka maendeleo ya kiroho, hamuwezi kufanikisha hilo kama hamzingatii katika kutimiza ahadi zenu za baiat mlizofanya na Imamu wa zama.

Alisema sababu nne zimetajwa kwa ajili ya wanawake kuolewa ikiwa ni pamoja na mali yake, uzuri wake, ukoo wake na dini yake. Hata hivyo, Mtume Mtukufu Saw amesema kwamba kigezo cha dini ndicho muhimu zaidi. Alisema ili kufu iweze kupatikana binti pia anatakiwa kuwa na shauku ya kumpata mwenzi ambaye ni mchamungu. Hivyo, wanaume nao wanatakiwa kujitahidi kuwa wema ili waweze kupata wanawake walio wema.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema Allah ametukumbusha kuzingatia taqwa ili kuwepo na kizazi chema na kuongeza kuwa mahangaiko ya leo yangeweza kupungua kama mafundisho haya ya Qurani Tukufu yangefuatwa. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema msiyafuate kama vipofu mataifa ya Magharibi. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kiwango cha kuvunjika kwa ndoa ni kikubwa hususan katika mataifa ya magharibi ambapo pia ndoa zingine ni za mikataba ya muda mfupi. Hivyo, ili kuongoka hatutakiwi kujiingiza katika giza bali tujaribu kujirekebisha.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema utafiti uliofanywa hapa Uingereza katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita umebaini kuwa zipo sababu nyingi zinazosababisha khula au wanandoa kutengana. Alizitaja sababu hizo kuwa ni pamoja na lugha mbaya inayotumiwa baina ya wanandoa, kukosa subira, familia kuingilia kati, kukosa uvumilivu na kutosema ukweli, mathalani kudanganya kuhusu masuala ya elimu. Kama ndoa hizi zisingeingiliwa na familia, zisingalivunjika haraka. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema wakati mwingine mama wakwe huwapiga mabinti wanaoolewa na vijana wao, hili ni jambo baya sana ambalo pia husababisha ndoa kuvunjika, hata jamaat inapochukua hatua dhidi ya jambo hili haipewi ushirikiano. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa zipo sababu nyingi zinazosababisha kuvunjika kwa ndoa lakini sababu kubwa ni kukosekana kwa taqwa. Alimwomba Allah ajaalie hekima na kuwawezesha wanaume na wanawake kutekeleza hilo. Amin.

Ahmadiyya itaendelea kupeperusha bendera ya Islam duniani

Na Mwandishi wetu

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) amesema kuwa jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya itaendelea kupeperusha bendera ya Mtume Mtukufu (Saw) duniani kote.

Akitoa hotuba ya kufunga Mkutano wa Mwaka wa 45 wa Uingereza uliofanyika kwenye viwanja vya Hadeeqatul Mahdi, Alton, nje kidogo ya jiji la London, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) baada ya kusoma Sura Al-Faatiha alirejea aya ya 41 ya Sura Al-Ahzaab (33:41): Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Mungu na Muhuri wa Manabii. Na Mwenyezi Mungu ndiye Ajuaye kila kitu.

Katika hotuba hiyo, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa siku hizi maadui wa Ahmadiyya wamekuwa wakizungumza maneno mengi hasa baada ya tukio la Waahmadiyya kuuawa huko Lahore, Pakistani lililotokea mnamo tarehe 28 Mei, 2011. Alisema amekuwa akipokea barua kutoka kwa watu mbalimbali wakiwamo wanafunzi wa shule na vyuo mbalimbali wakimweleza jinsi wanavyoathirika na mateso ya Waahmadiyya hususan tukio la Lahore.

Alisema kuwa mambo haya yamekuwa yakifanyika kinyume na ubinadamu mbele ya Serikali huku polisi wakishuhudia. Alibainisha kuwa imani ya Waahmadiyya kwa Mtume Mtukufu (Saw) ni kubwa kuliko inavyodhaniwa. "Mkitaka kututesa sawa, tunajitolea maisha yetu. Sisi waahmadiyya tunamwamini Mtume Mtukufu (Saw) zaidi pengine kuliko jinsi waislamu wengine wanavyomwamini", alisema na kuwataka maadui wa Ahmadiyya kufungua macho na masikio yao, na kuongeza kuwa "dhana ambayo watu wanayo kuwa sisi hatumwamini Mtume Mtukufu (Saw) kuwa ni Khatama Nabiyina si sawa. Watu hawaelewi maana sahihi ya Khatama Nabiyina vinginevyo wasingeendelea kuwatesa Waahmadiyya."



Bendera ya Jamaat Ahmadiyya ikipepea juu huku ikizungukwa na bendera za mataifa mbalimbali kama ishara ya Jamaat Ahmadiyya kuiongoza dunia.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alifafanua kuwa Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba Allah amemuonesha miujiza kwa sababu ya Mtume Mtukufu (Saw). Mtume Mtukufu (Saw) alipewa muujiza kuhusiana na elimu kama inavyoelezwa katika Sura Al-Jumu'a aya 3 hadi ya 4 (62:3-4):

3. Yeye ndiye Aliyemwinua Mtume katika watu wasiojua kusoma, atokaye miongoni mwao, anawasomea Aya Zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hekima, na ingawa kabla kwa hakika walikuwa katika upotevu dhahiri
4. Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao; na Yeye ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

Masihi Aliyeahidiwa (as) alidai kuwa Mtume Mtukufu (Saw) hakusoma shule lakini alipewa muujiza na kwamba Waakhariyna Minhum (wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao), ikiwa na maana ya kwamba miujiza hii itaendelea hata baada ya Mtume Mtukufu Muhammad (Saw). Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema hakuna mwislamu atakayefaidika mpaka aamini juu ya Khatama Nabiyina yaani aamini kuwa Mtume Mtukufu (Saw) ni mbora wa manabii wote. Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba mafanikio aliyoyapata ni kutokana na kumpenda na kumfuata kwa ukamilifu Mtume Mtukufu Muhammad (saw) na si vinginevyo. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema mamula na wapinzani wa Masihi Aliyeahidiwa (as) wanapaswa kutafakari jinsi ujaji wa Masihi wa Musa (as) unavyofanana na ujaji wa Masihi wa Mtume Mtukufu Muhammad (Saw). "Kuja kwa Masihi Issa a.s ilikuwa ni baada ya miaka 1400, vivyo hivyo, kuja kwa Masihi wa Mtume Muhammad (Saw) yaani Seydna Ahmad (as) ilikuwa ni baada ya miaka 1400. Tafakarini hapa", alisema.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa katika Sala na hususan kila rakaa waislamu huendelea huomba wanaposoma Sura Al Faatiha: ***'Ihdina swiratwa lmustaqhiyma, Swiratwa lladhiyna an-amtaalayhim'*** yaani "Utuongoze njia iliyonyooka, Njia ya wale Uliowaneemesha". Hali inayoonesha kuwa ni kuomba kuendelea kwa uhai wa dini ya Islamu na kwamba huu ni ubora ulioje wa mafundisho haya ya Islamu. Aidha, aliendelea kuwahoji wapinzani kuwa kama mtu anapata ufunuo na habari za ghaibu, huyo tumuitaje kama sio Mtume? Alifananisha kitendo cha Mwenyezi Mungu kuendelea kuleta ufunuo kwa umma wa waislamu ni sawa na bustani inayoendelea kumwagiliwa maji ili iendelee kupata uhai. "Tutegemee nini kwa bustani hii ambayo haimwagiliwi maji (ufunuo), si itakauka na kubakia miti kwa ajili ya kuni?", alihoji.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliwaonya magaidi kutowafuata mamulah mithili ya vipofu. Alisema mamulah wamekuwa na uhusiano na magaidi kwa ajili ya kupata manufaa ya kisiasa.

Akihitimisha hotuba yake iliyochukua takriban saa moja na dakika 20, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema tuiombee dunia kutokana na matatizo yanayotokea hivi sasa ikiwemo ugaidi. Alisema kuwa tukio la watu 76 kuuawa nchini Norway hivi karibuni limemfanya akumbuke tukio la waahmadiyya kuuawa huko Lahore, Pakistan mwaka uliopita.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema: "Kwa kuwa tunaelewa heshima ya Mtume Mtukufu (Saw), tutaendelea kujitolea maisha yetu. Kila Muahmadiyya anajitolea maisha yake kwa sababu ya kumpenda Mtume Mtukufu (Saw). Tupo tayari kujitolea kila kitu kwa ajili hii na kamwe hatutarudi nyuma. Bendera ya Mtume Mtukufu (Saw) itaendelea kupeperushwa dunia nzima kupitia Jamaat hii."

480,000 wajiunga na Ahmadiyya, vituo vipya 121 vyaanzishwa

Na Mwandishi wetu

Takribani watu 480,000 duniani kote wamejiunga na Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya katika kipindi cha mwaka uliopita (2010/2011).

Akihutubia katika siku ya pili ya mkutano wa kimataifa wa 45 wa mwaka (Jalsa Salana) katika viwanja vya Hadeeqatul Mahdi, Alton, nje kidogo ya jiji la London, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alielezea kwa muhtasari maendeleo ambayo Jamaat Ahmadiyya imeyapata katika mwaka uliopita huku akifafanua kwa kina jinsi Jamaat Ahmadiyya ilivyopiga hatua takriban katika kila nyanja.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema wakati idadi hiyo ya watu wakiwa wamejiunga na Imamu wa zama, zaidi ya watu milioni 85 huko Amerika ya Kaskazini wamefikiwa na ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya kuhusu amani kwa njia mbalimbali. Alizitaja njia hizo kuwa ni pamoja na kubisha hodi nyumba kwa nyumba, kwa njia ya kielektroniki na matangazo ya mabango. Aidha, alisema kuwa watu wengine mamilioni barani Ulaya, Asia, Australia na Afrika wamekifikishiwa ujumbe unaohusu msimamo wa Islamu juu ya uaminifu wa mtu kwa nchi yake.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kwamba Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya imeenea katika nchi 200 duniani. Kiongozi huyo wa waaminio alizitaja Chile na Barbados kuwa miongoni mwa nchi ambazo Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya imeanzishwa katika siku za hivi karibuni.

Waislamu Waahmadiyya mmoja mmoja au ujumbe uliowakilisha nchi husika na wawakilishi wengi kutoka serikalini walisafiri ili kuhudhuria Mkutano wa Mwaka wa Kimataifa wa Uingereza kutoka zaidi ya nchi 50 duniani.

Alisema, kwa kipindi cha miaka 27 iliyopita- tangu mwaka 1984 wakati Jumuiya wa Waislamu Ahmadiyya ilipopigwa marufuku kufanya shughuli zake za kidini nchini Pakistani, Jumuiya hiyo imeweza kuenea katika zaidi ya nchi 109.

Kuna zaidi ya maeneo 1,118 duniani yamekubali wito wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya. Aidha, jamaat mpya 839 imeanzishwa rasmi.

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) akiwahutubia waumini.

Alisema Sierra Leone inashika nafasi ya kwanza ambako zimeanzishwa zaidi ya jamaat mpya 145 ikifuatiwa na Mali jamaat mpya 57 na ya tatu ni Nigeria kulikoanzishwa Jamaat mpya 54.

Imeripotiwa kuwa nchini Niger machifu wengi wa vijiji wamejiunga na Islamu Ahmadiyya sambamba na wafuasi wao.

Katika mwaka uliopita, Jamaat Ahmadiyya imeongeza idadi ya misikiti mipya 419 duniani kote, idadi hiyo ikihusisha pia maeneo 298 ambako makundi ya watu wamejiunga.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alitangaza kwamba idadi ya nyumba za wabashiri za Jamaat Ahmadiyya sasa zimeongezeka hadi kufikia 2,325 ambapo kwa mwaka huu vimeongezeka vituo 121.

Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya tayari imekamilisha uchapishwaji wa tafsiri ya Kurani Tukufu katika lugha kuu zipatazo 70 duniani, na kwa hivi sasa tafsiri ya Qurani tukufu katika lugha nyingine zaidi ya 15 ipo katika hatua za mwisho kukamilika, alitangaza Khalifa Mtukufu (a.t.b.a).

Katika kipindi cha mwaka 2010, mahubiri yalifanyika kwenye maeneo ya vijijini katika nchi 50 kwa lengo la kuhuisha baiats na kueneza tena ujumbe wa amani.

Zaidi ya baiats (watu) milioni moja waliokuwa hawana mawasiliano na Jamaat waliweza kupatikana na kurejea, alisema Kiongozi wa waaminio.

Watu wapya waliweza kujiunga na Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya katika maeneo mbalimbali baada ya kukatishwa tamaa na viongozi wao wa dini (wasiokuwa waahmadiyya) ambao hawakudiriki kutoa msaada wowote katika maeneo ambayo waislamu wanataabika.

Akielezea kuhusiana na mahubiri, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alitoa mfano unaosisimua kuwa katika nchi moja, mtu mmoja alikuwa akimkashifu Seydna Ahmad (as), mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya waislamu Ahmadiyya. Mtu huyo ambaye alikuwa akitoa lugha ya matusi katika mjadala uliokuwa ukiendelea ndani ya gari

Endelea uk. 5

Kiongozi wa Ahmadiyya akutana na wanafunzi

Na Jamil Mwanga, London Uingereza



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) (mwenye kilemba), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wanafunzi wa Jumuiya hiyo wanaosoma katika Vyuo Vikuu nchini uingereza. Wa pili (kutoka kulia waliosimama) ni bw. Jamil Mwanga, mwandishi wa habari hizi.

Kiongozi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani,HadhratMirzaMasroor Ahmad (a.t.b.a) hivi karibuni amekutana na wanafunzi wa fani mbalimbali wa jumuiya hiyo ambapo wanafunzi hao waliweza kunufaika na baraka za kukutana na kiongozi huyo mtukufu.

Mkutano huo ulioandaliwa na uongozi wa Khuddam hapa Uingereza, ulifanyika kwa nyakati tatu tofauti katika ukumbi wa msikiti wa Fazl, London, washiriki wakiwa ni wanafunzi wanaosoma fani mbalimbali wa Shahada ya Kwanza, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu kutoka kwenye vyuo vikuu mbalimbali hapa Uingereza.

Mwandishi wa habari hizi alikuwa miongoni mwa washiriki, ambapo alipata fursa ya kuhudhuria kikao cha kwanza ambacho kiliwahusisha wanafunzi wa fani ya sayansi ikiwa ni pamoja na Uhandisi na Sayansi ya Kompyuta.

Katika kikao hicho, mada mbili zilizotayarishwa na wanafunzi wanaosoma Shahada ya Uzamivu (PhD) zinazohusu sayansi na utafiti ziliwasilishwa mbele ya Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) na ambapo yeye binafsi aliweza kuchangia kwa kutoa maoni na pia kuwapa fursa washiriki nao kufanya hivyo.

Mapema, wakati alipokuwa akiingia kwenye ukumbi wa mkutano, hata kabla ya kupata taarifa ya utangulizi kutoka kwa kiongozi wa vijana waahmadiyya Uingereza (Sadr Khuddam), Fahim Anuer Sahib, Khalifa

Mtukufu (a.t.b.a) alibaini kuwepo kwa mwanafunzi mmoja mwenye asili ya Afrika na kutaka kumfahamu mwanafunzi huyo kuwa ametokea nchi gani. "Umetokea wapi, na unasoma nini hapa Uingereza?", aliuliza Khalifa Mtukufu (a.t.b.a).

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) ambaye amewahi kukaa Afrika katika nchi ya Ghana kwa zaidi ya miaka minane (kabla hajachaguliwa kuwa Khalifa, Aprili, 2003) na ambaye pia amewahi kuzuru Tanzania Mei, 2005, alifurahi kumwona mwafrika na hususan mtanzania katika kikao hicho. Mara kadhaa, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) amekuwa akikaririwa akisema kuwa anawapenda sana waafrika. Mapema kabla ya kikao, baadhi ya wanafunzi walisema kwamba Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) hufurahi anapokutana na watu wenye asili ya Afrika, hivyo iwapo atakuona katika mkutano basi utarajie lazima ataongea nawe kwanza.

Hii ni mara ya tatu tangu mwaka 2009 ambapo Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) amekuwa na kawaida ya kufanya mkutano na wanafunzi wa vyuo vikuu hapa Uingereza kila mwaka kwa lengo la kuzungumza nao, kutoa mwongozo, ushauri wa tafiti mbalimbali lakini zaidi ya yote wanafunzi hao kupata baraka na maombi ya kiongozi huyo wa kiroho.

Kikao hicho ambacho kilianza kwa usomaji wa Qurani Tukufu, kilihudhuriwa na wanafunzi wapatao 35 na kudumu kwa takriban saa moja, na kilimalizika kwa maombi ya kimya yaliyoongozwa na Khalifa Mtukufu (a.t.b.a), kabla ya washiriki wote kupiga picha ya pamoja na kiongozi wao mpendwa.

Uongozi wa Ahmadiyya Songea wamtembelea Mkuu wa Mkoa

Adamu Nindi - Songea-Mapenzi ya Mungu



Mkuu wa mkoa wa Ruvuma Mh. Said Thabiti Mwambungu (kushoto) akipokea zawadi ya vitabu vya Dini ya Kiislam kutoka kwa Mbashiri wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Mkoa wa Ruvuma Sheikh Abid Mahmood Butt

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mh. Sadi Thabit Mwambungu ameyataka Madhehebu ya Dini kuendelea kutoa mahubiri yenye kuleta amani na utulivu na kuwaomba waumini kuiombea Tanzania.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mh. Said Thabiti Mwambungu ameyasema hayo baada ya kutembelewa na ujumbe kutoka Jumuiya ya Waislam Waahmadiya ukiongozwa na Sheikh Abid Butt. Mkuu wa Mkoa Mh. Said Thabit Mwambungu amesema viongozi wa dini wakiwa na msimamo wa dini kwa kutoa mahubiri yenye mafunzo kwa waumini wao. Nchi haiwezi kuingia kwenye machafuko.

Viongozi wa dini wana uwezo wa kuonyesha vipaji vya waumini wao wenye roho ya Mungu wanavyo changia kuleta amani. Amesisitiza kwa viongozi wa Dini kuhumiza waumini wao kushiriki kazi za kuleta maendeleo huku wakiendelea kuomba amani kwa nchi yao.

Sheikh wa Ahamadiya Abid Baht amesema shabaha ya kuwepo kwa watu katika nchi ni kuzitii serikali zilizopo katika madaraka na kuhakikisha watu wanaishi kwa amani bila kumwaga damu. Kumwagika kwa damu kunatokana na shetani kuteka mioyo ya waumin. Jumiyya ya Waislamu ya Ahamadiyya itahakikisha kuwa ina endeleza amani na utulivu uliopo.

Jumuiya ya waislamu Waahmadiya inahudumia waumini wake katika kutoa huduma zifuatazo: Elimu, Afya na Uchumi.

480,000 wajiunga na Ahmadiyya, vituo vipya 121 vyaanzishwa

Inatoka uk. 4

moshi, aliomba kuoneshwa ishara. Baada ya kuteremka kutoka kwenye gari moshi mtu huyo aligongwa na gari na kuwa ndio ishara aliyotaka kuoneshwa. Tukio hili lilifanya watu kumkubali Imamu wa zama na kujiunga na Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya.

Akizungumzia kuhusu mchango wa televisheni ya MTA kwa maendeleo ya Jamaat Ahmadiyya, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema tafsiri za lugha mbalimbali zinapatikana kupitia MTA. Aidha, watu wanaweza kutazama MTA kupitia mfumo wa simu za mkononi (mobile system) popote duniani na kuongeza kuwa hata katika simu za iphones watu wanaweza kutazama MTA. Alisema watu wamekuwa wakijiunga na Jumuiya Ahmadiyya kwa kutazama MTA. Alitoa mfano wa nchi kama Benin ambako watu wanasifu jinsi uzuri wa Islamu unavyoelezwa kupitia televisheni hiyo. Vilevile, nchini Norway mtu mmoja alitaka kufuta televisheni ya MTA lakini mwishowe alibaini kwamba inafaa na akawa na uwezo wa kujibu madai yanayotolewa dhidi ya islamu. Mtu huyu aliamua kurejea katika islamu kutokana na MTA. Alisema pia baadhi ya watu hupata njozi za kweli kwa kutazama MTA na hivyo kujiunga na Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya.

Akihitimisha hotuba yake iliyochukua takriban saa mbili na dakika 10, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alirejea maneno ya Masihi Aliyeahidiwa (as) akiwaonya wapinzani (Mullah) kuwa Jamaat Ahmadiyya imeanzishwa na Allah hivyo hawapaswi kuichezea. Aidha, alimwomba Allah awape hekima viongozi hawa wapinzani pamoja na wafuasi wao.

Matukio ya Jalsa Salana yamerushwa moja kwa moja kutoka Hadeeqatul Mahdi (Alton, UK) kupitia televisheni ya Kimataifa ya MTA inayorusha matangazo yake kwa saa 24. Matangazo ambayo pia yanapatikana kwenye video kupitia mtandao wa intaneti katika MTA. TV.

Bustani ya Washairi

UJIO WA MUBARAKA:

Kutoka toleo lililopita

61 Mola Aliwajalia, wakapata mwelekeo
Katikati ya Tabora, Mola katoa eneo
Maombi wakayatoa, kumpelekea Dio
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

62 Na Dio wa serikali, idhini kawatumia
Hali yake wasijali, samahani alitoa
Uchafu ulikithili, mahali hapo sikia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

63 Jukumu la serikali, watumishi kutolewa
Wasafishepo mahali, na uchafu kuondowa
Paka safika kwa kweli, kila mtu hakujuwa
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

64 Ujenzi wa msikiti, kipimo kikatolewa
Msingi wa Msikiti, kuchimbwa ukaanziwa
Waumini madhubuti, walisimama sawia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

65 Serikali mkoloni, kazi ilijitolea
Pamwe nao waumini, hatamu kushikilia
Mawe kuweka begani, mbali sana walitoa
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

66 Mafundi wa msikiti, wetoka serikalini
Walishiriki kwa dhati, kwa dhati yao moyoni
Walichonga maboriti, kwa hakika yao fani
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

67 Wahmadiyya jamani, walishiriki pamoja
Walionyesha imani, mshikamano wa haja
Kwa baraka za Manani, kazi lipata faraja
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

68 Serikali ilituma, mafundi wajerumani
Waliokuwa mateka, wa vita vya kikoloni
Mwingereza ninasema, kadhalika Jerumani
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

69 Mwaka wa elufu moja, mia tisa wasikia
Arobaini nataja, na nne namalizia
Tulizipata faraja, Mubaraka kwelezea
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

70 Kwa furaha alitaja, kumaliza msikiti
Na jina akalitaja, "ALFAZL" thabiti
Kupata nyumba faraja, makini twajizatiti
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

71 Tarehe ya ufunguzi, maulana alitoa
Tarehe kumi na nne, Desemba naelezea
Ni mwaka elufu moja, na mia tisa sikia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

72 Na sasa namalizia, ni arobaini na nne
Siku hiyo wasikia, ikawa ya ufunguzi
Watu walihudhuria, bila hata ya ajizi
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

73 Siku hiyo wasikia, gharama alizitoa
Za mchango wa Jamia, kwa kila Mwanajamia
Ni elufu thelathini, na tano naongezea
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

74 Mia moja themanini, na tisa naendelea
Nazo senti themanini, hesabu iliishia
Hiyo yote ni thamani, ya michango ya Jamia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

75 Michango ilitolewa, wakaribu na wambali
Ndugu wahapa Tabora, Darisalama sikia
Tanga nao Kampala, Nairobi na Mombasa
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

76 Sasa ninaelezea, gharama yote halisi
Ilikuwa thelathini, na tatu hizo elufu
Sifuri na thelathini, na sita nakuarifu
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

77 Thelathini nazo saba, nazo pia malizia
Senti hizo ni sambamba, hesabu zakamilisha
Ntakutajia namba, ni ngapi zimebakia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

78 Elufu mbili sikia, mia moja hamsini
Shilingi tatu wekea, zitie arobaini
Senti tatu nafungia, mahesabu mkononi
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

79 Mabaki ya mkononi, tarifa alizinadi
Kuwa tuna madhumuni, kuijenga maridadi
Nyumba iliyomakini, ya hapa msikitini
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

80 Ratiba ilitolewa, ya wageni waalikwa
Kumi unusu sikia, kitini wamekalia
Kumi na arobaini, Kuruani ilisomwa
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

81 Msomaji Kuruani, Amri Abedi likua
Mubaraka ni makini, Inchaji wa Jamia
Mengi aliyabaini, ubora Ahmadiyya
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

82 Na sifa zilitolewa, na wageni mbalimbali
Akiwemo wa Mkowa, Mkuu wa serikali
Nyingi sifa alitowa, kwa jengo lilokamili
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

83 Shughuli likamilika, saa kumi na mbili
Arobaini dakika, na sita kuwa kamili
Mengine nimeyaruka, kuyatoa ni muhali
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

84 Inchaji wa Jamia, Shekhe wetu Mubaraka
Mchango alichangia, kwa Kamishina Mkoa
Si mwingine ni Foster, mia tatu alitoa
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

85 Fedha hiyo wasikia, ni pole kwa majeruhi
Vitani waliumia, na wengine kufariki
Pisi alifurahia, kwa mchango wenye haki
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

86 Salaamu zapongezi, kweli zilimiminika
Kutoka kwa viongozi, mbalimbali wa sifika
Wakiusifu ujenzi, msikiti wa baraka
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

87 Idadi ya viongozi, waliotuma salamu
Arobaini na tatu, walizituma kwa hamu
Sikia hizo pongezi, ziliishika hatamu
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

88 Haikua si rahisi, kila mtu kumtaja
Kwa jina lake halisi, samahani nazitoa
Mnisamehe kwa jinsi, kama haipo faraja
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

89 Ndugu zangu wasifika, twaanza toka gizani
Ujio wa Mubaraka, wafungua zetu mboni
Na mengi yenye baraka, yapenya hadi nyoyoni
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

90 Kazi imekamilika, ya ujenzi msikiti
Isilamu wasifika, mje kwenye msikiti
Ibada kuitamka, kwa nia yako ya dhati
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

91 Shekhe wetu Mubaraka, hakika litufikia
Kaingia Tanganyika, kwa zake njema hisia
Mcha Mungu msifika, ni mpole kwa tabia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

92 Kazi yake ilofata, kufasiri Kuraani
Kufasiri kwa nukuta, kwa Kiswahili makini
Haikuwa na utata, kaifanya kwa yakini
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

93 Miaka ilimchukua, kumaliza kazi hii
Hakika ilimuia, ugumu wa kufasiri
Hata hivyo nakwambia, alifikia mwishoni
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

94 Kazi hii nisikia, ilikuwa ngumu sana
Miaka ilimchukua, mpaka kumalizia
Miaka tisa sikia, kwa kazi alitumia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

95 Elfu moja tisa mia, na hamsini na tatu
Kazi yake nakwambia, kilele ikafikia
Akawa kamalizia, hadharani kaitoa
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

96 Wengine walisaidia, akiwemo na Kaluta
Munawari naye pia, baraka walizipata
Muhanga walijitoa, wengine sikuwapata
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

97 Watu walifurahia, kufasiri Kuraani
Hongera kumtolea, Shekhe wetu Muhisani
Tafasiri kuitoa, itatutoa gizani
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

98 Wengi walifurahia, Mkombozi kaingia
Mengi tutayatambua, kwa pembeni yalowekwa
Kuwa hawakututoa, gizani walitutia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

99 Mafedhuli nakwambia, na kero waliitoa
Tafasiri kusemea, haramu kufasiria
Uharamu kwelezea, fafanuzi wakashindwa
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

100 Jambo likiwa sawia, Mola baraka Hutia
Mafedhuli kuishiwa, wakakosa la kutoa
Ujingani kubakia, kulalama wasalia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

101 Mipango aliitoa, vijana kwenda somea
Kuraani kusomea, Isilamu dini pia
Mahali kwa kusomea, kulikua ni India
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

102 Wa kwanza kuelekea, alikuwa ni Kaluta
Mwalimu wetu Amri, Abedi hana utata
Wamfahamu nakiri, msasa kwenda kupata
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

103 Wengine walofatia, watoto wa Jumuiyya
Yusufu wa Athumani, babuye Kambaulaya
Na Ali bini Salehe, wote walielekeya
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

104 Elimu wajipatia, ya Masihi Mwahidiwa
Ya Kuraani sikia, Kiarabu nacho pia
Ya Isilamu sawia, yote walikusanyiwa
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

105 Na wa kwanza kurejea, Amri ni shekhe wetu
Ni hamsini na sita, karibu mtoto wetu
Nyoyo zilifurahia, kufika na hapa petu
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

106 Kaluta mwana Amri, Abedi karibu tena
Twakushukuru kurudi, na nduguzo kuonana
Kwa elimu maridadi, twaingoja kupeana
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

107 Kaenda kama Mwalimu, karudi akiwa Shekhe
Akapewa na makamu, kwa nyingi mno sherehe
Msikiti maalumu, kiongozi kawa yeye
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

Endelea uk. 7

Kutoka uk. 6

108 Msikiti alopewa, ule wa Dalisalama
Uongozi lijaliwa, kwa baraka za Karima
Jumuia ilikuwa, mbele akaisukuma
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

109 Kazi zake Mubaraka, bado nazielezea
Vingi vitabu kandika, Masomo kisilamia
Kitabu cha Hijiria, kaandika kadhalika
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

110 Kafasiri kadhalika, vya Masihi Mwahidiwa
Watu tukafaidika, elimu tukajaliwa
Ujio wa Mubaraka, faida katuletea
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

111 Waliokwenda awali, na wao walirejea
Na nyadhifa mbalimbali, wapewa nao pia
Walikuwa ni wawili, misikiti wakapewa
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

112 Katika hawa wawili, mmoja aliteleza
Ni kijana Bwana Ali, masomo aliyabeza
Wakawa hawamkubali, idadi kaipunguza
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

113 Yusufu wa Athumani, tunaye hadi wa leo
Ni Shekhe wetu makini, aongoza wenzi wao
Asimamapo jukwani, fedhuli hurudi nyuma
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

114 Nakueleza ujue, ujio wa Mubaraka
Nacho chuo ukijue, kilifanya kwelevuka
Dalisalama penyewe ndipo alipo kiweka
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

115 Na sasa kimehamia, ni Morogoro mjini
Mahala na kutajia, ni Kihonda kijijini
Wanafunzi nakwambia, wafundishwa Kuraani
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

116 Mashekhe wa Afrika, na wao wamechangia
Nakwambia Mubaraka, na nyuma hakurudia
India kawapeleka, na dini watumikia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

117 Tunaye Shekhe Kaluta, Bakri ni jina lake
Daudi hana utata, Mmoto la babu yake
Ahamadi kakamata, Morogoro chuo chake
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

118 Kikosi umekijua, mbele kinatumikia
Jamia Ahmamadiyya, hakika yaendelea
Juhudi hizi wajua, giza zatuondolea
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

119 Ndugu zangu kwaherini, kituoni nimefika
Naiomba samahani, kwa yote niloandika
Yakiwa na punguwani, Ataridhia rabuka
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani.

120 Nawe wangu Mhariri, la heri nakutakia
Na Mola Akusitiri, juhudi kukongezea
Upate toa shairi, Jamia wapate jua
Allah Akujaze heri, afia njema upate.

Haruni Bundala Tabora
S.L.P 54, Kiloleni Tabora

UDHAIFU WAKO MJA

1. Kwa sifa na utukufu, hakika yuko Mmoja
Kang'arika hana kufu, si wa kwenda wala kuja
Katuumba wapungufu, ili tuishi pamoja
Udhaifu wako mja, ndio wako utukufu.

2. Chanzo chetu lainifu, tone moja la kutoja
Likawekwa paengefu, lisijepata kuvuja
Na mwisho wetu ni ufu, mzoga wenye kufuja
Udhaifu wako mja, ndio wako utukufu.

3. Mja jilinde upofu, ufike kwenye natija
Wacha mawazo potofu, kuwapendezesha waja
Muhofu Mola Latifu, Aloumba azwaaja
Udhaifu wako mja, ndio wako utukufu

4. Mja wewe ni hafifu, unayo mengi mauja
Ungajiona nadhifu, yako yatayokufuja
Kiri wako udhaifu, Mola Akuvishe koja
Udhaifu wako mja, ndio wako utukufu.

5. Dunia naikusifu, ikukweze madaraja,
Ikupambe kisanifu, ikwambie hutochuja,
Zama zitakukashifu, kufifia kwakungoja,
Udhaifu wako mja, ndio wako utukufu.

6. Ni wangapi maarufu, waloishi kwa kutoja
Wakasheheni mikufu, ya thamani na mikaja
Iwapi yao harufu, nani anayewataja
Udhaifu wako mja, ndio wako utukufu.

7. Walojipa utukufu, wa kuombwa kila haja
Umati ukawasifu, pasi kuuliza hoja
Wakafa ni wahalifu, hawana thamani moja
Udhaifu wako mja, ndio wako utukufu.

8. Viumbe usiwahofu, hawaachi kubwabwaja
Hawakosi hitilafu, wawe wa mama mmoja
Usijipe taklifu, ridhiko ndio faraja
Udhaifu wako mja, ndio wako utukufu.

9. Jitambue kiongofu, wewe si mja wa mja
Jiamini kinyoofu, usijezua vioja
Jipambe ukinaifu, japo huna afwaaja
Udhaifu wako mja, ndio wako utukufu.

10. Mja omba tahfifu, Molao ukimtaja
Yu Rahimu na Raufu, Mbebaji zako haja
Nenda Kwake kidhaifu, hiyo ndiyo kubwa hija
Udhaifu wako mja, ndio wako utukufu.

Ame

MANENO YA SEYDINA AHMAD A.S

Ili mpate yakini

Yakini ndicho kitu chenye baraka nyingi, kilicho lazima kwa kuokoka. Seyidna Ahmad amesema, "Enyi watu mumtakao Mwenyezi Mungu! Fungueni masikio na msikie kuwa hapana kitu kama yakini. Yakini peke yake ndiyo humfungua mtu katika madhambi. Yakini ndiyo inayotoa uwezo wa kutenda mema. Na yakini ndiyo imfanyayo mtu ashiki na mpenzi hasa wa Mola wake. Je! mnaweza kuacha dhambi bila yakini? Mnaweza kujikataza matamanio ya nafsi zenu bila nuru ya yakini? Au mnaweza kupata utulivu wa roho bila yakini? Au mnaweza kujibadilisha kweli kweli bila yakini? Je, iko kafara au sadaka yoyote chini ya mbingu yenye kuweza kuwaondoleeni dhambi? Au je damu isiyokuwa ya asili ya Isa mwana wa Mariamu inaweza kuwaokoeni katika madhambi.
Mtu huondolewa katika madhambi anapomjua kwa yakini Mwenyezi Mungu na uwezo Wake na malipo Yake. Hakika mzizi wa kila maasi ni ujinga. Mwenye kupata sehemu ya maarifa ya Mungu kwa yakini hawezi kuendelea kumwasi. Mwenye nyumba hawezi kukaa nyumbani mwake akijua kwamba tufani la maji linakuja kwenye welekeo wa nyumba yake; au moto umezunguka nyumba yake na umeiunguza ila pamebakia pahali padogo tu. Basi huyu hawezi kungojea katika nyumba ile. Kwa nini ninyi mmekaa katika hali yenu yenye hatari baada ya kujidai kuwa mna yakini kwa malipo ya Mungu? Basi fumbueni macho yenu na tazameni hukumu za Mungu zilizomo duniani. Na msiwe mapanya waendao chini ya ardhi; bali kuweni njiwa warukao juu na kupenda hewa ya mbinguni. Jihadharini msifanye madhambi baada ya kutubia, wala msiwe kama nyoka mwenye kujichubua gamba lake na ni nyoka vile vile. Yakumbukeni mauti siku zote, kwani yanawasogeleeni pole pole, lakini ninyi mmeghafilika nayo. Jitahidini mtakasike, sababu mtu hawezi kumpata Mtakatifu (Mwenyezi Mungu) mpaka ajitakase mwenyewe.
Lakini mnawezaje kupata neema hii? Mwenyezi Mungu amejibu Mwenyewe kama anavyosema katika Qur'an tukufu: Wasta 'iinuu bissabri wassalaat, yaani, Ombeni msaada kwa subira na kwa Sala" (sura 2:46) (Safina ya Nuhu).

TOLEO MAALUM

Bodi ya uhariri wa Gazeti la Mapenzi ya Mungu inapenda kuwatangazia wasomaji na wapenzi wote wa Gazeti hili kwamba; upo mpango wa kutayarisha toleo maalum la miaka 50 ya uhuru wa nchi yetu pamoja na miaka 75 ya Mapenzi ya Mungu.

Wasomaji na wapenzi wa 'Mapenzi ya Mungu' wanaombwa kuandika makala pamoja na kutunga mashairi juu ya mada hizo mbili.

Makala na mashairi yatumwe kwa:
Mhariri, Mapenzi ya Mungu,
P. O. Box 376, Dar es Salaam,
kabla ya tarehe 25/11/2011

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

MAWAIDHA YA MWISHO

Mkutano wa Mwaka wa 1911 ulifanyika tarehe 26-29 Desemba. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliuhutubia Mkutano kwa masaa mawili na nusu jioni ya Disemba 27. Matini yake ndiyo hii:

"Enyi mlioamini, Mcheni Mwenyezi Mungu ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwisha kuwa watiifu. Na shikeni kamba ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane; na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu mlipokuwa maadui naye Akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema Yake mkawa ndugu; na mlikuwa ukingoni mwa shimo la moto naye Akawaokoeni nalo. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyokubainishieni aya Zake ili mpate kuongoka. Na liwepo miongoni mwenu kundi linaloita kwenye heri na kuamuru kutenda mema na kukataza maovu, na hao ndio watakaostawi. Wala msiwe kama wale waliofarikiana na kuhitilafiana baada ya kufikia dalili zilizo wazi; na hao ndio watakaokuwa na adhabu kubwa (3:103-106)."

Katika hotuba yake alisisitiza baadhi ya mambo ambayo kwa kirefu ni haya:

''Mna wajibu gani kumhusu Mungu? Ni kwamba mshike vizuri itikadi za kweli, vitendo vyenu viafikiane nazo, na muwe wacha-Mungu. Ucha-Mungu unamhifadhi mtu katika shida na kumpatia raha. Mcha Mungu huondolewa hali zote za kulemewa. Anapendwa na Mungu na anaruzukiwa namna asivyotambua. Maombi yake hupokelewa na anajaaliwa ushindi juu ya maadui zake wanaoangamia. Milango ya elimu ya haki hufunguliwa kwa mcha-Mungu. Kwa hiyo, nasaha yangu ya kwanza ni: Muwe wacha Mungu, muwe wacha Mungu, muwe wacha Mungu kwa ajili ya Mungu. Muwe watii kwa Mungu sawasawa, mwisho wenu uwe katika hali ya kuwa watii kwa Mungu. Ibrahimu a.s., Mzee mtukufu, alihesabiwa kustahiki kupata baraka zote kwa sababu ya utii wa aina hiyo, kama ilivyosemwa: 'Mola wake Alipomwambia: Uwe mtiifu, akanena: Nimekwisha kuwa mtii kwa Mola wa walimwengu' (2:132). Kwa hiyo, kama nyinyi nanyi mwataka kujaaliwa baraka za kimbinguni, muwe wacha-Mungu. Ucha Mungu wa kweli huchipua katika Mwislamu wa kweli; kwa hiyo, kuweni Waislamu, na kifo kiwakuteni Waislamu.

Tena jumuikeni pamoja, na kwa nguvu ya pamoja shikeni kwa imara kamba ya Mungu, wala msifarakane. Nawasomeeni ile aya mara nyingine: 'Shikeni kamba ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane.' Basi shikamaneni na kamba ya Mungu nyote pamoja, wala msiiache kabisa. Katika Islam kamba ya Mungu ni Kurani Tukufu. Ma-Aria, Ma-Barahman, Ma-Sanatan, Wakristo, wasiomwamini Mungu na wapagani, wote hao wanaendelea kuivuta kamba hii upande wao kwa nguvu zao zote na wanataka kuivutia kwao kutia nguvu upande wao. Upande mwingine mwadai kuishika kwa nguvu hii kamba ya Mungu. Msiyaache madai hayo bila kuhakikisha ukweli wake. Tumieni nguvu zenu zote kwa pamoja kwa imara na ishikeni kwa nguvu, isije wapinzani wa Islam wakawashindeni katika kuvutana huku. Kuishika kwa imara inamaanisha kwamba muifanye Kurani Tukufu kuwa kanuni yenu na mwongozi wenu. Shughuli zote za maisha yenu ziwe sawa na mafunzo yake. Mambo yenu yote, kila mwendo wenu na kimya chenu kirekebishwe na Kitabu hiki Kitakatifu cha Mungu ambacho ni ponyo na mwanga. Nawafikishieni mara nyingine agizo la Mungu, lisikieni, na tegeni masikio barabara. Shikeni nyote kamba ya Mungu, wala msifarakane. Je, mwajua mkifarakana matokeo yatakuwa nini? Kamba itaponyoka mikononi mwenu, nanyi mtaondokewa nguvu yote, kama Mungu Mtukufu Alivyosema: 'Msigombane, msije mkatenguka mioyo na kupoteza nguvu zenu' (8:47). Mtavunjika na nguvu zenu zitatapanyika na maadui zenu watawashindeni.

Sikilizeni! Mimi ni Khalifatul Masihi, na Mungu Amenifanya *Khalifa*. Nilikuwa sitamani niwe *Khalifa*, lakini sasa kwa kuwa Mungu Amenivika joho hili, sipendi kabisa mafarakano. Sipendi asilani mwingiwe na mafarakano. Napenda kuodolea mbali sababu zote zile za mafarakano. Hamwezi kutambua jinsi wazo lenyewe la mafarakano linisumbuavyo mimi. Hamjui kipeo cha maumivu hayo; hamwezi kuyawaza. Napenda, na hii yategemea fadhili ya Mungu, ya kwamba nisisikie habari ya mafarakano yoyote kati yenu wala utengano, na kwamba niweze kushuhudia kwa macho yangu kwamba nyinyi ni mfano kwa kitendo wa agizo hili la Mungu: Shikeni kamba ya Mungu nyote, wala msitengane.

Nakariri, yule aliyekuwepo na asikilize na kuwafikishia wengine, epukaneni na ugomvi. Baada ya kufa kwangu mtakuwa na nafasi kubwa ya kugombana. Pengine mwafikiri nimekuwa *Khalifa* kwa urahisi kama Abu Bakr r.a. Hamtambui uhakika ulivyo, wala hamwezi kuelewa uzito wa wajibu niliobebeshwa, na mashaka yaliyosababishwa



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.

nao. Ni fadhili hasa ya Mungu kwamba nimewezeshwa kubeba mzigo huu mzito. Hakuna yeyote kati yenu anayeweza kuukisia barabara licha ya kuubeba. Je, anayepaswa kuwasimamia malaki ya watu aweza kulala usingizi kwa raha?

Nikisimama msikitini humu, Kurani mkononi, ninaapa ya kwamba sikutamani hata kidogo wakati wowote niwe mwalimu wa kiroho. Lakini hakuna ajuaye mpango wa Mungu. Amefanya Alivyopenda. Amewaunganisha nyote kwa mikono yangu, na Yeye Mwenyewe, si mmoja wenu, Akanivika joho la *Ukhalifa*. Ni faradhi yangu kulitukuza na kuliheshimu. Sitaki kwenu fedha au chochote kiwacho. Sijali mmoja wenu ananisalimia au hapana. Mpaka Aprili iliyopita nilikuwa nampelekea Maulawii Muhammad Ali michango yote mliyokuwa mnaniletea, lakini mtu fulani akamwongoza vibaya naye akasema fedha hizo ni mali ya *Anjuman*, naye akiwa katibu wa *Anjuman* ndiye mwangalizi wake. Ndipo nikaacha kumpelekea fedha hizo kwa kuthamini radhi ya Mungu, ili nione watafanya nini kuhusu habari hii. Wale wanaofikiri hivyo wamo katika kosa nao wamefanya hatia ya utovu wa adabu. Wapaswa kutubu; nakariri kwamba wapaswa kutubu. Wasipotubu watakuwa katika hali mbaya.

Sasa naweka kando fedha mnazoleta kwangu mimi binafsi na kuzigawanya ili kupata radhi ya Mungu. Siwategemei kwa mahitaji yangu wala kwa mahitaji ya familia yangu. Mungu Hakunifanya katu nimtegemee yeyote yule; Yeye Anipatia vya kutosha sana kutoka katika hazina Zake zilizofichikana. Isitoshe, bado nina uwezo wa kufanya kazi ya utabibu Aliyonijaalia Yeye. Zingatieni, nami narudia, sihitaji fedha zenu, wala siwaambieni mnipe. Mkiniletea chochote nakitumia katika njia ya radhi ya Mungu, jinsi nifikirivyo. Kitu gani, basi, kingeweza kuchochea utashi nafsini mwangu kwamba niwe mwalimu wa kiroho? Mungu Ametenda Alivyopenda; nyinyi wala yeyote mwingine hawezi kufanya chochote kuhusu jambo hili. Kwa hiyo jifunzeni kuheshimu mpango wa Mungu; ndiyo njia ya kujinyakulia baraka za Mungu. Hii pia ndiyo kamba ya Mungu iliyofungia pamoja mambo yenu yaliyokuwa yametawanyika. Ishikeni kwa imara.

Zingatieni vizuri kwamba nyinyi hamna madaraka ya kumwondoa *Khalifa*. Kama mkiona ndani yangu jambo fulani mnalofikiria ni kosa, niambieni kwa adabu. Ni Mungu Anayeweka *Khalifa*; hiyo siyo kazi ya binadamu. Mungu Alimfanya Adamu kuwa *Khalifa*, na pia Daudi. Tena Anaweka *Makhalifa* sawa na aya 24:56; nyinyi nanyi Akawafanyeni pia *Makhalifa*. Kama nimefanywa *Khalifa*, ndiyo kazi ya Mungu sawa na hekima yake na kwa faida yenu. Hakuna yeyote awezaye kumwondoa *Khalifa* aliyewekwa na Mungu. Hivyo yeyote kati yenu hana madaraka kuniondoa mimi. Kama Mungu Akitaka kuniondoa, Atanifisha. Afadhali mliache jambo hili mkononi mwa Mungu; nyiye hamna uwezo wa kuniondoa. Sidaiwi na yeyote kati yenu. Anaongopa yule asemaye amenifanya *Khalifa*. Naudhika nikisikia kauli hii kwamba hizi ni zama za Sheria na Bunge; Iran na Ureno na Uturuki zote zimeunda Mabunge. Nasisitiza kwamba yule anayeifikiria Jumuiya hii kuwa kama Bunge atubie kosa lake. Ni raha gani mnayofikiria ambayo Iran na nchi nyinginezo zimeletewa na Bunge? Wengi waliangamizwa chini ya enzi ya Muhammad Ali Shah, na wamfuatao nyuma wanaonywa-onywa. Je, Waturuki walilala kwa amani baada ya kuunda Bunge?

Nawakumbusheni mara nyinginekwambandaniyakurani Tukufu imefafanuliwa bayana ya kuwa Mungu ndiye Anayeweka *Makhalifa*. Alipomweka Adamu a.s., Akasema: Hakika Mimi Nitamweka *Khalifa* katika ardhi (2:31). Malaika wakaleta ukinzani, lakini huo ukawafaa nini? Someni Kurani mjue. Kama hiyo ilikuwa hali ya malaika na wakalazimika kuungama: Utakatifu ni wako! Hatuna elimu isipokuwa Uliyotufundisha (2:33); basi nyiye m nani kunikinza? Afadhali mjiangalie ndani ya vioo vyenu. Nakumbuka vizuri kauli ya mtu fulani: Bunge limeundwa katika Irani; hizi ni zama za kuunda kanuni. Mawazo kama hayo ni uasi na utovu wa heshima. Wanaofikiria hivyo walikwisha onyeshwa matokeo yake na ghera Ya Mungu katika Iran yenyewe. Narudia, wanapaswa kutubu hata sasa.

Naletewa fedha na nguo kwa ajili ya mayatima na mafukara. Fedha kama hizo namkabidhi Maulawii Muhammad Ali sawa na agizo: Wala msikaribie mali ya yatima (6:153). Pamoja na nguo wakati mwingine vitu vyenye thamani kubwa vinapokelewa. Nikamwambia mke wangu kuuza vitu hivyo na kutoka katika fedha hizo kutengeneza mavazi ya kawaida ili watu wengi zaidi wanaostahili wapate kusaidiwa. Mke wangu akauliza kwamba, je, anaweza kujinunulia baadhi ya vitu katika hivyo. Nikamwambia katu hapana, lakini wanawake wasio jamaa zetu wanaweza kuvinunua. Mara kwa mara watu wenye hali ndogo wanaoa, na mabibi arusi hupatiwa nguo na mapambo. Kisha kuna fedha ambazo naombwa zitumiwe sawa na maagizo yangu, ama kwa namna ambavyo marehemu fulani apatiwe thawabu yake. Fedha nyingine zinapokelewa kwa sadaka ya kawaida. Fedha nyingine zinatumwa kwa ajili yangu binafsi, nami najua hiyo hufanywa na mpango maalum wa Mungu.

Sikueleza hayo yote kujitetea. Mungu Anajua sana kwamba sithamini kibali chenu au kutokubali kwenu au kunichukia. Nimewaambieni isije mkafanya dhambi ya kudhania vibaya. Mimi sihitaji fedha zenu. Hata katika zama za uhai wa Masihi Aliyeahidiwa nilikuwa naletewa fedha kama hizi nami nikakubali. Nawaambia hayo, kwani nawatakia heri. Sina hofu hata kidogo ya yeyote kati yenu; namhofia Mungu pekee. Msifikirie vibaya. Kama nimo kosani, niacheni kosani. Katika umri huu kama sijajifunza kutoka katika Kurani Tukufu, mtanifundishaje? Hali yangu ni kwamba nikiendelea kuketi miguu yangu yaniuma; nasimama kuwahutubia, kwani Mtume Mtukufu alitoa hotuba akisimama. Basi nisikilizeni kwa ajili ya Mungu, kwani nawafikishieni agizo Lake: Ishikeni nyote pamoja kamba ya Mungu, wala msifarakane.

Akiongea na mgonjwa mmoja, tarehe 11 Juni 1912, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alinena:

"Katika kila kazi utaratibu huweza kuwekwa, isipokuwa katika kazi ya utabibu. Mjenzi anaweza kuchukua jukumu la kumaliza ujenzi wa jengo katika muda maalum; karani anaweza kuahidi kutayarisha taarifa katika siku kadha, mshonaji aweza kusema atatoa suti siku fulani; lakini tabibu hawezi kusema atamponya mgonjwa katika muda fulani, ingawaje baadhi ya matabibu wajinga wakati mwingine wanadai hivyo. Tabibu hodari hadiriki kutoa madai kama hayo. Mimi wakati mwingine napata dawa kutoka China, lakini ni mwangalifu sana hata kwamba hadi sasa sijaijaribu dawa yoyote katika hizo zilizo nyingi nilizopata kwa bidii kubwa na kwa bei ghali, kwa mgonjwa yeyote, kwani tabibu yeyote hajaniambia matokeo ya majaribio yake mwenyewe ya hizo wala njia ya kuzitumia. Siandiki mimea au dawa ambazo hazipatikani kwa urahisi."

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

NABII ISSA A,S.ALIKUFA NA WALA HATORUDI DUNIANI

Ustadh Issa Ally Malenge,
Bujumbura, Burundi.



Ust. Issa Ally Malenge, Mwalimu wa Jamaat Ahmadiyya Bujumbura, Burundi

Hakika kifo cha Nabii Issa a.s, ni miongoni mwa mambo ambayo yanatutofautisha sisi Waislam Waahmadiyya na Waislam wengine. Sisi Waislam Waahmadiyya tunaamini kuwa Nabii Issa a.s, alikuwa ni Nabii wa Allah, na alitumwa kwa wana wa Israel. (61:7) Aliishi kati ya watu wake akiwa ni Mtume wao, alipata maudhi mengi kutoka kwa watu wake, na hata walitaka kumuuwa msalabani lakini Mwenyezi Mungu alimuokoa. (4:158). Na alipokamilisha kazi yake ya utume, na muda wake ulipotimia alikufa kama walivyokufa Mitume wengine kabla yake. Hapa chini nitatoa dalili kutoka ndani ya Qur'ani kuthibitisha madai haya.

DALILI YA KWANZA

Na Mwenyezi Mungu atakaposema Ewe Issa Bin Mariam! Je,wewe uliwaambia watu; Nishikeni mimi na mama yangu kuwa waungu wawili badala ya Mwenyezi Mungu? Atasema :Wewe ndiwe Mtakatifu, hainipasi mimi kusema yale ambayo sina haki (ya kusema); Kama ningalisema bila shaka ungalijua; Unayajua yaliyomo nafsini mwangu,

lakini mimi siyajui yaliyomo nafsini mwako; Hakika wewe ndiwe Ujuaye sana mambo ya ghaibu. (Al-Maaida 117).

Mwenyezi Mungu atamwuliza Nabii Issa Bin Mariam a.s., kama ni yeye ndiye aliyewaambia watu wamshike yeye na mama yake kuwa waungu wawili badala ya Mwenyezi Mungu, mambo haya ataulizwa siku ya kiyama kama aya inavyosema:

Hii ndiyo siku wasemao kweli utawafaa ukweli wao. (Al-Maida:120). Majibu ya Nabii Issa kwa Mwenyezi Mungu kuhusu swali aliloulizwa yanapatikana katika aya ya (118): ***Sikuwaambia lolote ila yale Uliyoniamuru: ya kwamba mwabuduni Mwenyezi Mungu Mola wangu na Mola wenu; na nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa kati yao lakini uliponifisha Wewe ukawa Mchungaji juu yao, na wewe ni shahidi juu ya kila kitu.***

Hakika Nabii Issa a.s., anasema katika jawabu lake kuwa yeye alikuwa ni mchungaji na mlinzi wa watu wake alipokuwa kati yao, na alitengana nao kwa sababu ya kifo kwa ushahidi wa kauli yake kuwa ***(WAKUNTU,ALAYHIM SHAHIIDAM,MAADUMTU FIIHIM FALAMMAA TAWAFAYTANII KUNTA ANTA RAQIIBA ALAYHIM) na nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa kati yao Lakini uliponifisha Wewe ukawa Mchungaji juu yao (Almaidah 118).***

Masihi Issa Mwana wa Mariam hakujua kuwa watu wake walikufuru baada yake hata wakamfanya kuwa mungu. Hii ni dalili ya wazi kuwa Nabii Issa a.s. alikufa na wala hatorudi duniani kama wanavyo dhani baadhi ya watu. Kwani kama tuamini kuwa Masihi Issa a.s. yupo hai mbinguni na atarudi hapa duniani kuvunja misalaba na kuuwa nguruwe na kuowa na kuzaa, basi ni lazima tukiri kuwa jawabu la Nabii Issa mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya kiyama litakuwa ni la uongo. Atamjibu vipi Mwenyezi Mungu kuwa hakujua chochote kilicho endelea na hali ya kuwa alikuja duniani mara ya pili na kuwashuhudia Wakristo Wakimuabudu? Na haiwezekani Nabii wa Mwenyezi Mungu aseme uongo mbele ya Allah, tena siku ya kiyama. Hivyo kwa mujibu wa aya hii Masihi Issa Mwana wa Mariyam a.s. alikwisha fariki na wala hatorudi duniani kwani Mwenyezi Mungu anasema:

Na ni haramu kwa mji tuliouangamiza ya kwamba wao hawatarejea. (21:96).

Kwa hiyo bishara zote zinazoonyesha kurudi Nabii Issa a.s, mara ya pili duniani zitakuwa na maana ya kudhihiri kwa mtu mwingine ambaye atakuwa ni mfano wa Nabii Issa a.s. Mwenyezi Mungu anasema: **Na anapotajwa Mwana wa Mariyamu kwa namna ya mfano ndipo watu wako wanaupigia kelele.** (43:58).

Nabii Issa wa Banii Israeli alikuja kusadikisha Taurati ambacho kilikuwa kitabu cha sheria kilicholetwa na Musa a.s. Hivyo hivyo katika umma huu atakuja mtu ambaye atasadikisha kitabu cha Qur'ani ambacho ni kitabu cha sheria kilicholetwa na Mtume Muhammad s.a.w. Huo ndio mfano wa kurudi Nabii Issa mara ya pili hapa duniani. Hata Nabii Elia Wayahudi walikuwa wanaamini kuwa alipaa mbinguni kama inavyoaminiwa leo juu ya Nabii Issa. (2 Wafalme 2:11). Pia waliamini kuwa atarudi kama wanavyoamini leo hii baadhi ya watu juu ya Nabii Issa a.s, (Malaki 4:5). Lakini Nabii Issa mwenyewe aliwaambia Wayahudi kuwa Yohana M'batizaji ndiye Eliya mwenye masikio na asikie. (Mat.11:14~17:12)ilisemwa atakuja Eliya lakini alikuja Yohana, tena kwa kuzaliwa na si kushuka kutoka mawinguni. Huu ni ujumbe wa wazi kutoka kwa Nabii Issa a.s, kwa wale wote ambao wanatumai kuwa ipo siku atashuka kutoka mbinguni. Kamwe hatashuka.

DALILI YA PILI

Dalili ya pili inapatikana katika Sura ya tatu, Mwenyezi Mungu anasema: ***(Kumbukeni)Mwenyezi Mungu aliposema: Ewe Issa, kwa yakini mimi nitakufisha na nitakunyanyua kwangu, na Nitakutakasa na (masingizio ya) wale waliokufuru, na nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru mpaka siku ya Kiyama; kisha marudio yenu yatakuwa kwangu, ndipo Nitawahukumuni katika yale mliyokuwa mkikhitilafiana. (3:56).*** Wapo baadhi ya wafasiri wa Qurani tukufu ambao wamejaribu kupotosha maana ya aya hii; wanadai kuwa maneno (*Innii mutawaffiika warafiuka ilayya*) Yaani Mimi nitakufisha na Nitakunyanyua kwangu; hayana maana hiyo bali maana yake ni; Mimi nitakutimizia muda wako wa kuishi na nitakunyanyua kwangu, hii ndio tafsiri ambayo imeshikwa na baadhi ya wafasiri wa Qurani. Unaweza kuyaona haya katika tafsiri ya Shekh Abdallah Swaleh Farsii. Wametoa tafsiri hiyo ili kuilinda imani yao juu ya uhai wa Nabii Issa huko mbinguni. Lakini hata hivyo hila yao hiyo imeshindwa kabisa, ukweli wa Qurani kuwa Nabii Issa alikufa uko wazi mno kwa yule atafutaye ukweli. Hebu jiulize katika nafsi yako, mtu anayetimiziwa muda wake wa kuishi anakuwa katika hali gani? Bila shaka anakuwa amekufa.

Neno *Tawaffa* linapokuwa limetumika kutoka *baab tafa'uul,* Mwenyezi Mungu akiwa ni mtendaji (*Faailu*) na mwanadamu akiwa ni mtendwaji (*maf'uulu*) na kisha neno tawaffa lisifuatiwe na karina (neno la kuongezea maana zaidi kama vile 'usiku' au 'kulala'), basi siku zote linamaanisha kufa tu. Wanachuoni wakubwa na Mufasiriina wa Qur'ani tukufu kama Ibn Abbas, Imam Maliki na Imam Bukhari na wengine wengi, wanakubaliana na kanuni hii niliyoieleza.

Katika Masimulizi yaliyomo ndani ya Sahih Bukhari, Ibn Abbas r.a, akitoa maelezo ya aya ya 118 katika sura ya 5 anasema (*Mutawafiika ay, mumiituka*) yaani Mutawafiika maana yake ni nitakufisha. Bukhari kitabu tafsiri, tafsiri ya aya ya 118 ya sura ya 5. Pia Fat'hul Bayaani kinasema "hao mufasiriina ambao wamejaribu kutia maana nyingine katika neno Tawaffa linavyotumika kwa maana hiyo, wamefanya hivyo kwa sababu ya kusadiki kwao kuwa Yesu amepandishwa mbinguni hai waila neno hili halina maana nyingine isipokuwa maana ya kuchukua roho au kufisha. Na neno hili Tawaffa limetumika pahala pasipopungua 25 ndani ya Qur'ani tukufu na ni pahala pawili tu ndipo limeleta maana tofauti na kifo, katika sura ya (6:61) na (39:43). Kwa nini katika aya hizi mbili neno Tawaffa limebadili maana? Ni kwa sababu limefuatwa na karina (neno la kuongezea maana zaidi).

Baadhi ya aya ambazo Allah Amelitumia neno Tawaffa ni katika sura ya Al-Baqara, Mwenyezi Mungu akizungumzia juu ya wanawake waliofiwa na waume zao, Anasema ***(Walladhiina <u>yatawaffauna</u> min'kum, wayadharuuna az'waaja wwaswiyyata lliaz'waajihim).*** Na wale <u>wanaofishwa</u> miongoni mwenu na kubakisha wake, wawausie (warithi) kwa ajili ya wake zao (2:241). Pia dua waliyofundishwa Waaminio ili wawe na mwisho mwema, ili siku watakapo kufa wawe katika hali njema inapatikana katika Sura Aal-Imraan, Allah anatufundisha tumuombe kwa maneno haya <u>Watawaffanaa</u> ma'al-ab'raar, yaani <u>Utufishe</u> pamoja na watu wema.

Katika kitabu cha Bukhari kuna maelezo ya Bibi Aisha r.a, ambaye ni mmoja wa wake wa Mtume Muhammad saw, yanayoelekeza mahala alipofia Mtume Muhammadi saw, yeye anasema: *Tuufiya Nnabiyyi s.a.w. fii baytii,* Kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alifia katika nyumba yangu. Bukhari juzuu ya tatu uk 59. Angalia neno alilolitumia Bi Aisha kuzungumzia kifo cha nabii wa Allah, Ni Tawaffa. Kwa wale wasomi wa lugha ya Kiarabu kama utasoma kamusi mbalimbali za Kiarabu utakuta neno Tawaffi limepewa tafsiri ya kutoka roho. Baadhi ya makamusi hayo ni Aqrabul-Mawaarid, kamusi hiyo inasema kuwa: Tawaffa Llahu fulaanaa, ay'qabadhwu ruuhahu. Kuwa Mwenyezi Mungu anapo mfanyia mtu Tawaffa huwa amemuondoa roho yake. Katika Lisanul-Arab mmeandikwa, *Tawaffaahu Llahu –Idhaa qabadhwu nafsahu;* yaani Mwenyezi Mungu anapo mfanyia mtu Tawaffa ni wakati anapomtoa Nafsi yake. Kwa hakika neno Tawaffa lina maana ya kufa tu linapokuwa limetumika kutoka katika mlango wa Taffaul, Hata baadhi ya Mashekhe waliowahi kupinga tafsiri hii walikuja kukubali tafsiri hii baada ya kubainikiwa na ukweli, mmoja wao ni sheikh Abdalla Swaleh Al-farsy, ambaye aliipinga tafsiri hii katika tafsiri yake ya Qur'an kwa Kiswahili. Lakini baadae katika gazeti lake la Sauti ya haki alikiri kabisa ya kuwa kwa mujibu wa aya hii na nyingine nyingi zinazopatikana ndani ya Qur'an Tukufu, Nabii Issa as, amefariki kama mitume wengine waliopita kabla yake. Huu ndio ukweli wa Qur'an ambao kila mtafuta haki inabidi aufuate. Wayahudi walikasirishwa mno na mahubiri ya Nabii Issa, hivyo wakatumia kila njia ili kumzuwiya katika harakati zake za kueneza imani ya kweli, walipoona wanashindwa kumzuwia ndipo walipopanga kumuuwa, tena wamuuwe kifo cha laana ili kila mtu ashuhudiye kuwa alikuwa ni mtu mwongo na mlaaniwa. Katika hali hiyo Nabii Issa a.s, alianza kuyaona maisha yake yapo hatarini, wakati Fulani aliwahadharisha wanafunzi wake kuwa wasimwambie mtu ye yote kuwa yeye ni alikuwa yule Yesu Kristo (Mat.16:20).

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya yaweka Historia mpya

Kutoka uk. 12

Asubuhi yake baada ya kutuandalia chai, Sadr alianza kikao kwa maombi ambacho pia kilihudhuriwa na Khuddam kutoka Jamaat ya Suluti.

Sadr alimtaka katibu kusoma ajenda za kikao ambazo zilihusu taarifa ya Ijtmaa na Shura, Maendeleo ya ujenzi wa jengo la Tanzim na kusimamisha uongozi kwenye matawi ya Namtumbo na Suluti. Sadr aliwataka khuddam pamoja na kazi nyingi za kilimo bado wana wajibu wa kujitoa kwa ajili ya Jamaat na hilo ndilo jukumu letu kubwa kwa sasa. Walifikishiwa maazimio ya shura iliyopita ambayo utekelezaji ndio hasa mkakati wetu kwa sasa uliopata ridhaa ya Khalifa Mtukufu, hivyo tuna wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa tunatekeleza suala la michango, tabligh na tarbiyat kikamilifu.

Baada ya mazungumzo ya kina vijana walishika ahadi ya kuyatekeleza hayo kwa jitihada zao zote na watatumia kila maarifa waliyonayo kuhakikisha kuwa wanabadilisha hali yao na pia walimshukuru Sadr kwa kuchagua kuwatembelea na wamepata nguvu mpya.

Kikao kilifungwa kwa maombi yaliyoongozwa na Mwalimu Rashid Issa Nyoni na kututakia safari njema.

Safari ya kuelekea Ligunga ikaanza na baada ya kupita pori kubwa lililotuchukua masaa zaidi ya manne tukafika Jamaat ya Ligunga wakiwa chini ya Mwalimu Yusuf Mambo. Na hapo tukamkuta pia Mwalimu wa kanda hiyo Mwalimu Rashid Yakini akitusubiri kwani sasa Sadr alikuwa anaingia kwenye himaya yake.

Baada ya mapokezi mazuri kabisa yaliyojaa kila aina ya faraja na bashasha ya ajabu kwani kuna Ansurullah aitwae Mzee Simama wakati tunakumbatiana alikuwa na joto kali mwilini hadi nikamuuliza akaniambia nina homa na nimetoka kufanya operesheni hivi karibuni lakini niliposikia ugeni toka Makao Makuu unakuja nikasema hapana siwezi kulala nyumbani nitafika niwaone na niwasikilize. Mzee huyu alihudhuria Jalsa Salana ya mwaka juzi Dar es Salaam na ya mwaka jana hakuwahi kwa sababu ya maradhi. Haya ndiyo mapenzi ndani ya Jamaat yanapofikia kumtoa mtu mchozi si ya mchezo.

Hii ilifuatiwa na chakula ambacho itatuchukua pia muda mrefu kukisahau na wenyeji wetu walikuwa wamejipanga vilivyo.

Baada ya kusomwa Qur'an Tukufu na shairi zuri la kumkaribisha Sadr, ilifuatia risala murua iliyosomwa na Atfalul Ahmadiyya kwa umahiri wa hali ya juu.

Sadr alifungua kikao kwa kiapo cha khuddam na kama kawaida yake aliwaomba Ansurullah waendelee kukaa.

Akamtaka katibu asome ajenda na kuwaeleza madhumuni ya safari yetu na kuwaomba khuddam wawe wasikivu kwani mambo tuliyokuja nayo ni mengi na ya muhimu kwa maendeleo ya Tanzim na Jamaat yetu kwa ujumla.

Maelezo ya kina yalitolewa na taarifa ya Ijtmaa na Shura, maendeleo ya ujenzi wa ofisi zetu Kitonga Dar es Salaam na kuunda safu ya uongozi katika tawi la Ligunga.

Sadr Sahib alisifu mchango wa Mwalimu Yusuf Mambo katika Tanzim na mara zote amekuwa ni kiungo muhimu kati ya tawi na Makao Makuu. Amemuomba Mwalimu aendelee kuwa hivyo katika siku zijazo.

Baada ya kusomewa maazimio ya shura iliyopita vijana wameonekana kuelewa na kupokea ujumbe na Sadr aliwaomba waendelee kutoa ushirikano wa hali na mali hasa katika mawasiliano kati ya tawi na Makao Makuu.

Katika maelezo yao walimtoa shaka Sadr juu ya ukimya walionao wakati wote wa maongezi yake, hii ni kwa sababu wanameza na kulitafakari kila neno na kilichobaki ni kwa Sadr kuona matunda kwa vitendo.

Sadr aliwatakia kila la kheri na kikao kilifungwa kwa maombi ya kimya yaliyoongozwa na Mwalimu Yakini na msafara ulielekea Tunduru mjini.

Tunduru mjini tulikuta kama kawaida khuddam walikuwa wanatusubiri na kwa kuwa tuliingia jioni sana walitupa muda wa kusali magharibi na baadaye tukaungana pamoja kwenye sala ya Insha.

Chakula cha usiku kilikuja kwa ajili yetu nacho kilikuwa ni cha aina yake na baada ya hapo tulielekea nyumbani kwa khuddam anaemaliza muda wake Bwana Omari Lisinge tulipata malazi na mahitaji muhimu kwa siku zote tulizokaa Tunduru.

Baada ya chai ya asubuhi kwa mwenyeji wetu safari ya Lukumbule ilianza tukisindikizwa na Mwalimu Yakini.

Tulikuta wenyeji wetu wakitusubiri kwa hamu kubwa na kama walivyo khuddam wengi tuliowapitia walikuwa hawaamini kama kweli Sadr anakuja hadi walipomuona ndipo hasa wakaonyesha furaha yao.

Tulikuta wameandaa chai hivyo ikawa chai ya pili kwa asubuhi hiyo ambayo ilikuwa ya kukata na shoka. Baada ya kusalimiana na kutembelea baadhi ya maeneo muhimu ya kijiji cha lukumbule tulirejea kwa ajili ya kikao .

Kikao kilifunguliwa kwa usomaji wa Qur'an Tukufu na risala ya khuddam ilisomwa kwa Sadr Sahib.

Maombi ya kimya yalifanywa na kiapo cha khuddam kilifuatia na Sadr aliwataka khuddam tujitahidi kufanya kazi za Jamaat na kama ilivyosemwa kwenye risala kuwa tawi hili linajengwa na Khuddam na Atfalu Ahmadiyya na baadhi ya Lajna inabidi mfanye kazi ya ziada kuhakikisha mipango ya Jamaat inakwenda sawa.

Baada ya kumtaka katibu kusoma ajenda za kikao aliwataka khuddam wote tupange muda wa kufanya kazi za kujitolea yaani waqar amal. Hizi ni kazi zenye kutufanya tofauti kati yetu na wengine iwe bayana katika kutoa huduma.

Sadr aliwapa taarifa ya Ijtmaa na Shura, maendeleo ya jengo la Tanzim na uongozi wa Tanzim katika tawi la lukumbule, Makande na Kazamoyo na hiyo ni hatua muhimu kwenye kuimarisha Tanzim yetu.

Khuddamul walionekana kuwa wasikivu na makini na walisema kuwa wameyapokea yote waliyoambiwa na kumuomba Mwenyezi Mungu awafanyie wepesi katika utekelezaji wake.

Kikao kilifungwa kwa maombi ya kimya yalioongozwa na Mwalimu Suleiman Rashid ambaye baadaye alitutambulisha rafiki wa Jamaat wa pale lukumbule ambaye yeye ni mfuasi wa dhehebu la Ahl Qur'an. Bwana huyu aitwae Ust. Jabir ambaye alivutiwa na ujio wetu lakini kubwa ni jinsi kama Waislamu tunavyoweza kupanga mambo yetu hali iliyomfanya amuhadithie rafiki yake wa karibu ambaye ni Ahl Qur'an mwenzake .



Picha ya pamoja kati ya Wanajamaat wa tawi la Muhuwesi na uongozi wa Khuddamul Ahmadiyya taifa.

Taarifa zilizotufikia wakati tukienda mitamboni zinasema kuwa rafiki wa karibu wa Ust. Jabir amejiunga kwenye Jumuiya na amefanya baiat siku tatu tu baada ya kuondoka kwetu. Ni maombi yetu kwa Allah aendelee kumbainishia haki hii Ust. Jabir. Inshaallah.

Chakula cha mchana kiliandaliwa kama kawaida utamu wa chakula unamzidi mwenzie na tumbo kazi yake kupokea ili kupunguza chumvi wali kwa kuku ulikuwa mtamu basi itoshe.

Wenyeji wa lukumbule hawako nyuma walitutembeza maeneo muhimu kwanza nyumbani kwa Marehemu Mzee Mchemela na Sadr alitoa pole nyumbani hapo ambapo ndipo Jamaat ya Lukumbule ilipozaliwa na Sadr alipata nafasi ya kupiga picha ya ukumbusho. Halafu tukapelekwa kuona Kitonga ya Lukumbule eneo zuri lenye mikorosho mingi hapo ndipo tukaagana rasmi na wenyeji wetu, na kwa kuwa tukio hili la kupeana vibega lilifanyika hadharani ilikuwa ni jambo kubwa ambalo nadhani watu wengi wa lukumbule walitaharuki na kuvutiwa sana na ugeni wetu. Hadi Ust. Jabir alifikia kusema ingependeza ikiwa mngelala hapa leo. Safari ya kurudi Tunduru Mjini ikaanza kwa ajili ya kikao.

Sasa ilikuwa ni zamu ya Jamaat za Tunduru mjini kufanya kikao ambacho kilianza baada ya sala ya alasiri ambacho khuddam toka matawi ya Nakayaya, Kitanda na Naluwale walihudhuria.

Kikao kilifunguliwa kwa usomaji wa Qur'an Tukufu na kufuatiwa na kiapo cha khuddam.

Sadr Sahib alimtaka katibu kuwekambeleyakhuddamajenda za kikao na baadaye alianza kwa kuzielezea ajenda moja baada ya nyingine na kuwapata khuddam wote waliopo taarifa ya Ijtmaa na Shura, maendeleo ya ujenzi wa ofisi za Tanzim kitonga na umuhimu wa kuwa na viongozi katika matawi yote ili kuimarisha Tanzim yetu. Aidha Sadr alimuomba Mwalimu aendelee najitihada za kusaidia kupatikana kwa viongozi na muhimu kwa viongozi wakajenga nidhamu ya kutoa taarifa kila mwezi kwa Sadr na wajue kuwa Sadr anampelekea Khalifa Mtukufu taarifa kila mwezi. Kwa utaratibu huu ili kuimarisha Ukhalifa ni lazima kwa taarifa itumwe katika ngazi zote.

Sadr aliwashukuru Khuddam na kuwataka waimarishe timu ya mpira ambayo wameeleza kuwa wanayo na angependa kuona timu inakuja kwenye Ijtmaa. Inshallah.

Kikao kilifungwa kwa maombi ya kimya yaliyoongozwa na Bw. Omari lisinge ambaye pia ni rais wa tawi la Nakayaya na Khuddam anaemaliza muda wake. Usiku wake ni chakula na mapumziko tayari kwa safari ya kuelekea Muhuwesi.

Safari ya Muhuwesi iliaanza na kusindikizwa na mwenyeji wetu Mwalimu Yakini. Tulikuta Khuddam na Atfal mahiri kabisa waliongozwa na Takbira zilizovuma Muhuwesi karibu yote.

Moja kwa moja Qaid wa tawi la Muhuwesi Bwana Sandali Rajabu alimuongoza Sadr Sahib msikitini na kumsomea ratiba nzima ya tukio lililoanza kwa usomaji wa Qur'an Tukufu, shairi zuri la kumkaribisha mgeni, usomaji wa risala na tukio la kwa Atfalul Ahmadiyya kusoma kwa ghaibu baadhi ya hadithi toka kitabu cha hadithi arobaini za Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w). yalikuwa ni matukio mazuri yaliyonegesha kikao hicho na kutufanya tuone kweli tupo kwa Mzee wa Malezi na huyu ni Mwalimu Rajabu Sandali.

Baadaye alimkaribisha Sadr Sahib ili kuendelea na ratiba. Sadr aliwataka Khuddam na Atfalul Ahmadiyya wote kusimama kwa kiapo cha Khuddam. Sadr aliwaambia Atfal kuwa kipo kiapo cha Atfal na mambo yakiwa mazuri nanyi mtakuwa mnaapa kwa kiapo chenu na hili litakuwa ni jukumu la viongozi wa hapa wawasaidie.

Sadr alimtaka katibu kuwaeleza Khuddam ajenda za kikao na moja kwa moja aliwaeleza Khuddam lengo kuu la ziara hiyo ambayo kiratiba Jamaat ya Muhuwesi ndiyo kituo cha mwisho. Sadr alisema tumeanzia Jamaat za Iringa Mjini na leo tupo Muhuwesi Mkoani Ruvuma, hivyo tuna kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu katika hili.

Walipewa taarifa ya Ijtmaa na Shura na kuwaambia kuwa hiyo ni haki yenu kushiriki na haya waliyoyafanya Atfal basi waletwe kwenye Ijtmaa washindane na wenzao kutoka maeneo mengine ya nchi.

Sadr aliwafahamisha maazimio ya Shura iliyopita na kuwaomba kushirikiana na Qaid kuweza kuyatekeleza haya na kubwa zaidi ni kutoa taarifa kwa Sadr ili amtumie taarifa hiyo Khalifa Mtukufu.

Maendeleo ya ujenzi wa jengo la ofisi za Tanzim waliambiwa na kuelezea furaha yao ya hatua ilipofikia.

Sadr alimtaka Qaid wa tawi hilo kuunda safu ya uongozi ili kusaidia kufanya kazi za Tanzim na amtumie kwa idhini ya Majlis Amila na kumuomba Mwalimu Sandali atusaidie kuhakikisha Tanzim inasimama imara katika tawi.

Khuddam wa Muhuwesi walieleza furaha na kusema kuwa "kumbe Khuddam ina watu wazito namna hii na walionona nilidhani ni sisi wenye miili midogo", alisema Qaid wa tawi baada ya kuona baadhi viongozi walioambatana na Sadr walikuwa na vitambi na hawaonekani kuwa na shida hata kidogo.

Waliahidi kuyafanyia kazi yote waliyofikishiwa na kumuomba Sadr ikitokea anapanga ziara nyingine asisahau Jamaat ya Muhuwesi.

Na angalau awe anarudi baada ya miezi mitatu ili kuangalia aliyoyasema kama yanakwenda vizuri. Sadr alisema kufanya safari hizi kunategemea mfuko wa Tanzim na kwenye Shura ndio kwenye mipango inakopitishwa hivyo aliwataka wahudhurie Shura kupanga mipango ya Tanzim bila ya kusahau kutuma ajenda za Shura.

Kikao kilifungwa kwa maombi yalioongozwa na Mwalimu Sandali Rajabu. Sadr alipata nafasi ya kutembelea eneo la Jamaat na wao wamepata kitonga yao,eneo zuri lenye Mikorosho mizuri liko tayari kwa ujenzi wa Msikiti,ikafuatia kile ambacho nakiita kuwa ni dhifa. Tukaagana na wenyeji wetu na hapo ndipo Mwalimu Yakini tulipomuacha kwani msafara wa Sadr ulikuwa unarejea Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo ya Mikoa ya Nyanda za juu kusini, Sadr alipata nafasi ya kuwaeleza Khuddam nidhamu ya Tanzim kiuongozi aligawa katiba ya Tanzim kwa kila tawi alilokwenda yenye lengo la kuwafanya khuddam waifahamu Tanzim yao vizuri zaidi kuliko wakati wowote uliopita.

Pia alitoa fomu maalum za kutolea taarifa ya kazi za tanzim amabazo inabidi zijazwe kila mwezi na kuzituma Makao Makuu, Sadr alisisitiza kuwa hicho ndicho kiungo muhimu kati ya tawi na Makao Makuu na Markaz. Ikitokea kiongozi anakuwa hayupo ni jukumu lake kuhakikisha kuwa kuna mtu anamwacha anafanya kazi hiyo. Ikitokea Qaid anakuwa hayupo kwa zaidi ya siku kumi na tano basi analazimika kumfahamisha Sadr ili kazi za Tanzim zisisimame.

Sadr pia alitoa mwito kwa Khuddam kuchangia jengo la Tanzim na aligawa fomu kwa matawi yote ili wachangie mifuko miwili ya saruji na wale wenye uwezo zaidi watajaza fomu nyingine kwa michango ya ziada.

Katika ziara hiyo Sadr aliwaambia khuddam kuwa, Tanzim yetu imekuwa ya kwanza miongoni mwa Tanzim nchini kutoa jengo lake na kuisaidia Jamaat kulitumia kama sehemu ya Shule hivyo kuwataka khuddam waendelee kuwa mbele katika kufanya kazi za Jamaat popote pale kwenye tanzim bila ya kujali kama Tanzim zingine zinafanya au hazifanyi, sisi tuwe wa kwanza kufanya mambo mazuri kwani ni kazi yetu kuisadia Jamaat. Alisisitiza Sadr.

Tumuombe Mwenyezi Mungu aifanye ziara hii ya Mikoa ya Nyanda za juu kusini kuwa ni yenye mafanikio. Amin.

Jalsa Salana, fursa ya wema, elimu na maendeleo kiroho

Kutoka uk. 12

mmoja ana majukumu na wakati mwingine rasilimali ni finyu. Ukarimu ni sifa ya wema ambayo inatakiwa ijenge heshima na udugu kati ya mgeni na mwenyeji na kuendeleza uhusiano wa upendo kati yao, lakini mtu anapozidisha muda wa kukaa inaweza kuleta matokeo kinyume na haya.

Mafundisho bora ya Islamu yanabainisha kuhusu mambo madogo madogo na kutoa maelekezo ya jinsi mtu anavyotakiwa kuenenda katika mazingira haya. Maelekezo ya jinsi ya kukabiliana na mambo madogo madogo matokeo yake ni kufanikiwa na kufikia wema kwa kiasi kikubwa sana. Miongoni mwa madhumuni ya kufanya Mkutano wa Mwaka kama ilivyoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa (as) ni kuimarisha udugu miongoni mwa washiriki na kujenga jumuiya yenye upendo. Uhusiano huu bora wa kidugu na umoja unaweza tu kujengwa kwa kuwa watiifu sana kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Mtukufu (Saw). Hivyo, kila mgeni hana budi kuongeza kiwango chake cha utii ili kupiga hatua zaidi kuliko kurudi nyuma.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) pia aliwakumbusha wageni kuwa malazi yanayotolewa na Jamaat ni kwa ajili ya muda mfupi. Wageni ambao wamedhamiria kukaa kwa majuma mawili au matatu wanatakiwa kuheshimu ahadi yao na kwamba kama wanataka kuendelea kukaa humu nchini kwa zaidi ya kipindi hicho, wanatakiwa kuandaa mipango mbadala na kufuata kanuni zilizowekwa na Nidhamu ya Jamaat, kwa sababu rasilimali za Jamaat ni finyu, na malazi yanayotolewa wakati wa Jalsa yanatakiwa pia kwa ajili ya madhumuni mengine.

Aidha, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisimulia hadithi nyingine isemayo: hairuhusiwi kwa mgeni kuendelea kukaa hadi akawa chanzo cha dhambi kwa mwenyeji wake. Je, hii inawezekanaje? Mwenyeji, ambaye anaweza akawa hana rasilimali za kutosha, anaweza akawa amekopa fedha ili kumwezesha mgeni wake kukaa raha mustarehe. Kama mgeni akizidisha muda wa kukaa kwenye makazi ya mwenyeji wake, na mwenyeji asiwe na uwezo wa kurejesha fedha alizokopa, basi anakuwa ni mwenye dhambi. Aidha, kama mgeni anakaa zaidi ya siku alizokaribishwa, mwenyeji wake anaweza akapatwa na hasira au kutaabika na kuanza kulalamika kuhusu wageni wake, hapo pia inakuwa ni dhambi. Hivyo, mgeni anatakiwa kujaribu kuelewa hali hii na asichangie kumfanya mwenyeji wake kupata dhambi. Kama mgeni na mwenyeji wote wakitimiza wajibu wao, basi hakuna yeyote atakayepata dhambi.

Ni msaada wa Mwenyezi Mungu kwa Jumuiya Ahmadiyya kwamba 99.99% ya waahmadiyya wanasikiliza ushauri unaotolewa na wanatii maagizo. Wachache wanaokaidi wanatakiwa pia kufuata miongozo wanayopewa. Mtume Mtukufu (Saw) hali kadhalika, alikuwa akiwasihi masahaba zake na kuwapa ushauri kutokana na jinsi alivyobaini tabia isiyofaa ya mmoja au wawili miongoni mwao, na si kutokana na tabia ya kundi kubwa la masahaba. Mfano mzuri ni uhusiano wa Muhajir na Ansar, ambapo Ansar walikuwa hasa ndio wenyeji kwa kuwaandalia wageni wao chakula kizuri na nyama, na Muhajir wakawa wageni hasa kwa kuwaomba wenyeji wao wawaoneshe mahali soko lilipo ili waweze kujinunulia wao wenyewe na sio kuwa mzigo kwa wenyeji wao. Mtume Mtukufu (Saw) alitoa maagizo haya mara kwa mara – mosi ili kujenga mafundisho mema kwa masahaba zake na pia wale wapya waliojiunga na Islamu. Qurani Tukufu inasema: "Basi, shindaneni katika mema" (2:149). Kulingana na fundisho hili la Qurani, ipo hamasa katika mioyo ya waaminio ili kupiga hatua. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alikumbusha kwamba wale wanaopiga hatua katika mambo haya wanatakiwa pia kuangalia nyuma ili kuwavuta wale waliobakia nyuma na kuwaleta kwenye mstari ili kila mmoja katika jamii afanye jitihada ya kusonga mbele na waaminio waungane kama taifa moja. Maelekezo haya yanatolewa sio kwa nia ya kudhalilisha au kumkwanza yeyote, bali kujenga mafundisho mema kwa kundi lote kwa jumla.

Ushauri mwingine ambao Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliutoa kwa upande wa Ziafat (upokezi wageni) au Langar ni kwamba, ingawaje wageni wote wanapatiwa chakula cha aina moja, kuna nyakati ambapo baadhi ya wageni hupatiwa chakula tofauti; wale wenye mahitaji ya mlo maalum au wale ambao hawana ladha ya chakula cha Pakistani kutokana na historia ya tamaduni zao. Hivyo, kwa namna yoyote wageni wasitaabishwe na hilo. Hata hivyo, waandaaji hawatakiwi kujipikia mlo maalum kwa ajili ya matumizi yao binafsi. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliwakumbusha wote waliopangiwa majukumu mbalimbali kuwaheshimu na kutowakwaza wageni kwa mamna yoyote ile, hata kama itakusudiwa kuwa ni katika hali ya kufanyiana utani au mzaha. Wageni wahudumiwe mara zote kadiri ya ambavyo wangependa kujihudumia wenyewe. Hata hivyo, wageni hawatakiwi kutumia vibaya vyakula kwa kula kiasi wanachotaka na kumwaga kinachobakia. Wahudumu wasiwaharakishe wageni kuondoka kwenye eneo la kulia chakula bali waachwe wale kwa amani na kwa kasi wanayotaka. Hata hivyo, wageni pia wanatakiwa wakumbuke kuwa hawatakiwi kuendelea kuwepo katika eneo la kulia chakula baada ya kumaliza kula. Kumbuka kuwa wahudumu wana majukumu ya kutekeleza na wanahitaji muda wa kupumzika vilevile. Kwa hakika mtazamo wa wageni na wenyeji ndio utakaofanya mandhari kuwa nzuri kwa ajili ya wote kufurahia.



Jalsa Salana pia ni fursa ya watu kufahamiana na kudumisha udugu: Pichani ni miongoni mwa wajumbe walioshiriki Mkutano wa Mwaka wa Kimataifa wa 45, Uingereza. Kutoka kushoto ni Dkt. Imran Khan, Qaid Khuddam wa eneo la Kaskazini magharibi (Northwest Regional), Uingereza, Sheikh Fareed Ahmad Tabasam kutoka Tanga, Tanzania, Jamil Mwanga, mwandishi wa makala na Bw. David Stephen Bell, mwanajumuiya mpya aliyejiunga kutoka Manchester, Uingereza.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) pia alikumbusha kwamba shabaha kubwa ya Jalsa Salana ni kujenga uhusiano imara na Allah. Hivyo, wahudumu wote na wageni wote ni lazima wazingatie kwa makini kuhusu sala zao na pia kusali sala za nafali na kufanya maombi na dua, kwa sababu suluhisho la vikwazo vyetu, hususan katika kukabiliana na mateso ya maadui, linategemea ibada ya namna hii.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kwamba Jalsa inatoa fursa ya watu wengi kukutana na ndugu na marafiki zao ambao hawajakutana kwa miaka mingi. Watu hawa wanatakiwa wakutane wakati ratiba ya shughuli za Jalsa inapokuwa imesitishwa. Inatakiwa ikumbukwe kwamba watu wanatakiwa waepuke kujihusisha na mijadala isiyofaa na badala yake, wajaribu kumkumbuka Mwenyezi Mungu na wale waliotutangulia, na kufanya majadiliano mema na yenye heshima. Kuna nyakati ambapo uhusiano mpya huanzishwa wakati wa Jalsa; Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) tena alikumbusha, hususan wanawake, kwamba kipindi cha mapumziko wakati wa Jalsa ndicho kitumike kwa ajili ya madhumuni haya. Aidha, alisema watu wasikae na kuongea hadi usiku wa manane kwa sababu inakuwa ni vigumu au ni vigumu kabisa kuamka kwa ajili ya sala za asubuhi na nafali. Kumbukeni madhumuni ya kipindi hiki ni kujenga mazingira ya kiroho. Wanawake wanatakiwa hasa kukumbuka kwamba hili si tamasha la kidunia, hivyo kila juhudi inapasa kufanywa kupiga hatua kiroho na katika wema. Hii siyo nafasi ya kuonesha mavazi au mapambo. Wanawake wanatakiwa kuvaa mavazi ya heshima ambayo yanafunika urembo wao badala ya kuuonesha. Wanaume na wanawake wanatakiwa kuinamisha macho yao ili kunufaika kiroho na mkusanyiko huu wa Jalsa Salana.

Kuhusu maandalizi ya Jalsa Salana, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kwamba ulinzi mwaka huu umekuwa ni mkali zaidi. Hivyo, itatokea wageni wakatakiwa kupita kwa ajili ya ukaguzi na mabegi yao yanakaguliwa. Tafadhali, muwe wavumilivu kwa sababu hatua hizi zimewekwa kwa ajili ya usalama wenu wenyewe. Kila wakati mgeni atakapoingia kwenye ukumbi wa Jalsa, yeye pamoja na mabegi yake yatakaguliwa, kwa hakika mtatakiwa wenyewe kuyatoa mabegi yenu ili yakaguliwe. Tafadhali, zingatieni taratibu hizi kwa hiari na wala msilalamike. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) pia aliwaagiza wahudumu kuendesha ukaguzi huo wa kiusalama bila ucheleweshaji usio wa lazima ili shughuli za Jalsa ziweze kuanza kwa wakati. Uzio umewekwa kutenganisha mipaka ya uwanja wa Jalsa; hata hivyo, katika uzio huu inatakiwa awepo mlinzi kwani uzio peke yake hautoshi. Kila mtu aliyepo katika Jalsa Salana anatakiwa kutupia jicho lake sehemu inayomzunguka ili kubaini nyendo yoyote inayotia shaka. Mwaka huu, mipango imefanywa kwa ajili ya wazee na akina mama wenye watoto kuwatengea mlango wao tofauti wa kuingilia na ukaguzi ili wasicheleweshwe kuingia katika ukumbi wa Jalsa. Hata hivyo, uvumilivu bado unahitajika kwa sababu kadri muda unavyokwenda, foleni inaweza kuwa kubwa. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliagiza kwamba takbira zisitamkwe mara kwa mara; kwa hakika idara maalum inatakiwa kuwa na jukumu la kazi hii. Hata hivyo, pindi takbira inapotamkwa, inatakiwa ijibiwe kwa pamoja na kwa sauti. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliwakumbusha washiriki wote kubakia katika ukumbi wa Jalsa wakati wa hotuba na kuzisikiliza kwa vile ni kwa ajili ya manufaa yetu. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema uangalizi maalum uzingatiwe katika kudumisha usafi, hususan katika vyoo. Katika hali ya mvua, vyoo vinaweza kujaa matope. Wahudumu wanafanya kazi kusaidia usafi, lakini wageni pia wanakumbushwa kutekeleza wajibu wao. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) aliekeleza kwamba wale wanaofika kwenye ukumbi wa Jalsa kwanza wajaze nafasi zilizo mbele ili wanaochelewa wapate nafasi ya kukaa. Wanaochelewa hawatakiwi kuwaruka watu wengine ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi. Kwa hakika, inatakiwa kuhakikisha kwamba hakuna nafasi zilizoachwa wazi katika ukumbi wa jalsa.

Akihitimisha, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisisitiza umuhimu wa sala na kufanya maombi na dua katika muda wote wa Jalsa Salana. Allah atuwezeshe kutekeleza hayo, Amin.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

Dhul-Qa'dah 1432 AH | Oktoba 2011 | Tabook 1390 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat 'Aabis bin Rabii'ah r.a. aliyesema: Nilimwona Hadhrat Umar bin Khattab r.a. akilibusu jiwe, yaani jiwe jeusi, huko akisema: Natambua u jiwe usilonufaisha wala kudhuru. Na kama nisingelikuwa nimemwona Mjumbe wa Allah s.a.w. akikubusu nisingelikubusu. (***Bukhari***)

Kiongozi wa Ahmadiyya duniani asema:

Jalsa Salana, fursa ya wema, elimu na maendeleo ya kiroho

Na Mwandishi wetu

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a), alitoa hotuba ya Ijumaa katika viwanja vya Hadeeqatul-Mahdi, katika Mkutano wa Mwaka wa Jumuiya Ahmadiyya Uingereza. Khalifa Mtukufu a.t.b.a alisema kwamba katika hotuba ya Ijumaa iliyopita alitoa maelekezo hususan kwa wale Waahmadiyya ambao wanatekeleza majukumu muhimu sana ya kuwa wenyeji, kuwakirimu na kuwakaribisha wageni wa Mkutano. Aliwakumbusha wale wanaotekeleza majukumu mbalimbali kuwa Jalsa Salana ni mkutano uliobarikiwa sana, ambapo wanatakiwa kuonesha tabia ya ukarimu bila kujali ni idara gani wanayotumikia. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kwamba katika hotuba ya Ijumaa ya leo, angependa kusisitiza tena kuhusu wajibu wa wenyeji na wale waliopangiwa



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih V a.t.b.a.

kutekeleza majukumu mbalimbali. Aidha, alipenda kutoa maelekezo kadhaa kwa wageni wa Jalsa Salana, na zaidi ya hayo, kutoa baadhi ya maagizo ya kiutawala. Alisema kwamba, ingawaje maelekezo ya kiutawala yamechapishwa na kubainishwa kwenye programu ya Jalsa Salana, imebainika kwamba watu ama hawayasomi au hawayapi umuhimu unaopasa. Kwa namna yoyote, ni muhimu kuyarudia kama ukumbusho.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kwamba sisi kama waahmadiyya tumebarikiwa kwa kuwa wafuasi wa mtumishi wa Mtume Mtukufu Muhammad (saw) na kuungana na nidhamu ya Ukhalifa. Hivyo, pindi waahmadiyya wanapopewa maagizo na maelekezo, wanatakiwa wajitahidi sana kuyatekeleza kwa sababu kama hawatayafuata maagizo hayo, basi ni tofauti gani itakuwepo kati ya wanajumuiya Ahmadiyya na watu wengine. Allah ajaalie washiriki wote kupata mafanikio ya kiroho yatokanayo na Jalsa Salana.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisimulia hadithi ifuatayo: "Kwa anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho anatakiwa kumtendea wema jirani yake; na kwa yule anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho anatakiwa kumkirimu kwa zawadi mgeni wake. Mtu mmoja alimwuliza Mtume (Saw) ni zawadi gani hiyo. Mtume (Saw) akasema: zawadi inayotosheleza Kwa mchana mmoja na usiku mmoja. Ukarimu unaendelea hadi siku tatu. Kama ukiendelea zaidi ya hapo, basi ni sadaka kwa mgeni. Yeyote anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho anatakiwa ama azungumze lililo jema au akae kimya."

Sanjari na hadithi hii, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kwamba kwa hakika ni haki ya mgeni kufurahia ukarimu na malazi yanayotolewa na mwenyeji wake, lakini anatakiwa kukumbuka ukomo wake. Mwaminio wa kweli kamwe hatopendelea kupata sadaka, hivyo atatakiwa kukumbuka kwamba kukaa zaidi ya siku tatu kutahesabiwa kama sadaka. Haifai kwa mgeni kuzidisha muda wa kukaa na kuwa chanzo cha mzigo kwenye makazi ya mwenyeji wake kiasi hiki kwamba mwenyeji aanze kuhisi tabu na mahangaiko. Maisha hapa ni kwamba kila

Endelea uk. 11

Nini hasa maana ya Jihadi?

Kutoka toleo lililopita

Na moja katika ufunuo wangu uliotajwa katika Barahini Ahmadiyya miaka 20 iliyopita imesemwa "Annas samaawaati wal ardhwa kaanata ratqan fafataqnaahumaa" kwamba mbingu na ardhi vilikuwa vimeambatana kisha Tukaviambua" (Sura Anbiyaa aya 31). Maana yake ni kwamba mbingu na ardhi vimefungwa pamoja kama mzigo na vitu vyake vilikuwa vimefichwa. Katika siku za Masihi tumefungua mzigo huu na tukaziweka bayana siri zake. Mwishoni ikumbukwe ya kwamba nimeeleza kwa undani katika maandiko yangu kwamba desturi inayofanywa na Waislam ya kuwashambulia watu wa dini nyingine shambulio linaloitwa Jihad kwa hakika hiyo siyo Jihad ya Islam. Huo ni uvunjaji wa dhahiri wa amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na ni dhambi kubwa. Kwa sababu desturi hii imejikita mno miongoni mwa Waislam si jambo rahisi kuiondoa. Si ajabu wakaitafuta damu ya mtu anayewashauri juu ya kuacha jambo hilo.

Katika jazba yao wanaweza kuwa tayari kabisa kumuua mtu huyo. Mnaweza kufikiria mfano mmoja katika mnasaba huo. Mfano huo ni Amir wa Kabul ambaye nguvu zake miongoni mwa makabila ya Afghanistan haujawahi kufikiwa na Amir yeyote mwingine. Amir huyo awaite wasomi wa dini ili alete mdahalo, kwa kupitia mdahalo huu watu waweze kuelezwa juu ya makosa yao. Magazeti yaandikwe na wasomi hao katika lugha tofauti. Nina uhakika hatua hii ikichukuliwa inaweza kuwa na athari kubwa kwa watu. Taratibu munkar walio nao watu uliowashwa na Mamura unaweza ukapungua. Litakuwa ni jambo la kusikitisha iwapo Amir hatachukua hatua ya namna hii ambayo inaweza kusaidia kuleta mabadiliko katika jamii hiyo. Lakini kutojali jambo hilo kutaleta matatizo makubwa katika nchi ambayo yatakatokana na hao Mamura. Ni desturi ya Mamura wa siku hizi ya kwamba kwa kosa dogo tu basi mtu anaitwa kafiri

Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya yaweka Historia mpya

Kutoka toleo lililopita

Kikao kilianza kwa Usomaji wa Qur'an Tukufu na kufuatia na risala iliyosomwa kwa Sadr na walimueleza Sadr kuwa Mtu maarufu na Mwinyi wa kabila la Wayao alikuwepo kutupokea na kutusikiliza.

Sadr alianza kikao kwa kuwataka khuddam kutimiza wajibu na kuwaeleza taarifa za Ijtmaa na shura, maendeleo ya ujenzi wa jengo la ofisi za Tanzim Kitonga mjini Dar es Salaam na pia kuwafahamisha na kumuomba Mwalimu Maliki Sandali aisaidie Tanzim kuunda safu ya Uongozi na kumjulisha Sadr Makao Makuu. Lengo letu ni kuweka mtandao mzuri wa kitanzim nchi nzima na ukisha kuwa imara basi tutapunguza kuwasumbua walimu ila kwa sasa mtusaidie hili, alisema Sadr.

Kikao hicho kilichopata wawakilishi kutoka matawi ya Lusewa, Matepwende, Amani na mjumbe kutoka eneo la magazine ambapo Sadr alipata fursa kujibu maswali mbalimbali yaliyohusu malezi na umuhimu wa michango ndani ya Jamaat.

Kikao kilifungwa kwa maombi ya kimya na baadaye tukapata chakula kitamu sana. Sadr alipata muda kuangalia eneo la Jamaat ambalo walipewa na kijiji wakiambiwa kwa kuwa ni mbali basi watakuwa wamekomolewa, la haula! Khuddam wakachimba kisima chenye urefu wa futi



Picha ya pamoja kati ya Wanajamaat wa tawi la Namtumbo na uongozi wa Khuddamul Ahmadiyya taifa.

thelathini na saba na kuwafanya watu wote kufuata maji eneo la Jamaat na watu wamekata viwanja karibu na eneo kwa kufuata huduma hiyo muhimu. Kazi hiyo nzuri imeongozwa na Mwalimu Maliki Sandali. Mwenyezi Mungu Ampe nguvu zaidi. Pia wamejenga msikiti mdogo ndani ya eneo hilo walilolipa jina la kitonga namba mbili. Sadr Sahib alikabidhi mchango kidogo wa fedha kwa ajili kununulia misala ya msikitini.

Tukiongozwa na Amwenye yaani Chifu wa Kabila la Wayao ambaye kwa jina ni Abdallah Akwilombe alitupeleka kwenye ofisi za Serikali kusalimia na kujitambulisha na hali ya hewa katika Lusewa ilibadilika kwa muda huu mfupi. Amwenye amemuomba Sadr Sahib haja ya kufanya mhadhara mkubwa Lusewa ili Masheikh wa hapa wapate ujumbe huu. Amwenye bado hajajiunga na Jamaat ila tumuombee.

Tukaagana kwa bashasha kubwa tayari kwa safari ya Namtumbo.

Tulifika Namtumbo tukakuta khuddam walikuwa wanatusubiri japokuwa ni usiku, waliandaa chakula na kupata malazi mahala pazuri kabisa. Alhamdullilah.

Endelea uk. 10